KIKOMO

E. A MUSIBA

KIDOKEZO

Si kazi yangu kujishughulisha na makosa ya jinai. Nilishangaa kidogo Chifu aliponiamru nifuatilie tatizo la upungufu wa Almasi. Isingekuwa kwa sura aliyoonyesha, nilitaka kumwambia apeleke malalamiko yake kwa Kamishna wa Polisi au anipe uhamisho kwenda huko kama alikuwa hanihitaji katika idara yake. Siku hiyo alivaa sura ya kutisha na sikuwa na la kufanya ila kukubali.

Kulikuwa na ushahidi kwamba Almasi zilizouzwa katika masoko ya nje zilikuwa chache sana kulingana na kiasi kilichokuwa kimechimbwa kwa nini?.

Askari Polisi Joel amegusa chanzo cha uhalifu; akafa katika ajali ya ndege siku chache kabla ya kufunga ndoa na mchumba wake Amanda, na uhalifu ukaendelea.

Chifu alimtuma Jack Mbusile, mpelelezi wa kawaida. Lakini maiti yake iliokotwa ikielea katika Ziwa Victoria na uzito wa jambo zima ukawa umetambuliwa. Ndipo nikatumwa mimi Willy Gamba.

La hasha! Kama ungetumwa wewe nina hakika ungekimbia na kupotea kabisa! Lakini mimi sio wewe. Safari yangu ilinichukua katika miji ya Mwanza, Shinyanga, Maganzo na Songwa; na uvundo niliofichua ulisababisha umwagaji mkubwa wa damu na kuteketeza maisha ya watu wengi.

Yalikuwa mapambano makali na kila mmoja wetu alishangaa kuona ni nani alikuwa anaongoza uhalifu huu.

Ama kweli kikulacho ki nguoni mwako.

SURA YA KWANZA

Nilifika ofisini kwangu yapata saa mbili unusu. Gari langu lilikuwa limeniletea matatizo kidogo njiani. Katibu wangu nilimkuta tayari keshafika saa nyingi kama kawaida yake.

"Habari ya leo. Mbona umechelewa hivi?"

"Salama tu. Gari langu binti nafikiri niliuze maana siku hizi linanihunia sana".

"Lazima likuhunie, nalo unafikiri halichoki, maana linakata mitaa ya Dar es Salaam yote kila siku". Tukacheka.

"Kuna habari zozote?"

"Katibu wa Chifu alipiga simu na kuacha maagizo kuwa uende ukamuone Chifu mnamo saa tano na nusu, habari nyingine ndiyo mpigie Didi simu".

"Asante Luiza", nikaingia ofisi kwangu. Niliangalia majalada yaliyokuwa yakisubiri niyashughulikie kabla sijaenda kumuona Chifu hapo saa tano na nusu. Kufika saa nne nilikuwa nimeishayapitia majalada yote muhimu na kulikuwa na mawili kati yake ambayo ilinibidi niende nayo kwa Chifu kusudi niweze kuyazungumzia kabla sijaendelea mbele na matatizo yake.

Nilikumbuka kuwa ilikuwa inanibidi nimpigie simu Didi. Nilibonyeza simu kumuita Katibu wangu.

"Luiza nipigie simu kwa Didi".

"Sawa".

Muda si mrefu simu yangu ikalia.

"Huyo yuko kwenye simu".

"Halo, habari?"

"Nzuri, hujambo?"

"Sijambo".

"Nimekupigia simu asubuhi lakini ulikuwa bado hujafika, maana nyiye wazee hamchelewi".

"We, acha kunikoga nchi hii haina wazee wanaofanya hivyo. Ukifanya hivyo utaachishwa kazi".

Alicheka nami nikacheka.

"Je wasemaje?"

"Nina shida kidogo nilitaka kukueleza kuwa utokapo ofisini saa nane na nusu nipitie. Kuna jambo la maana sana ninalotaka kukueleza na kulifanya".

"Sawa mama. Hapana taabu. Mimi saa nane na dakika thelathini na tano juu ya alama napiga breki hapo".

"Nitashukru sana, kwaheri".

Nikakata simu. Nilikaa nikifikiria jinsi ya kumwelezea Chifu matatizo yaliyokuwa katika majalada haya mawili niliyokuwa nimeyaweka pembeni. Niliona nichukue notisi kidogo maana Chifu yeye huhitaji maelezo kamili. Saa tano na dakika ishirini na tano nilimwendea katibu wangu.

"Naenda kwa Chifu, chukua habari yoyote".

"saa sita na nusu naomba kwenda kumpeleka mdogo wangu hospitali, anaumwa".

"Kama nitakuwa nimerudi, lakini kama sijarudi usiondoke, kama kawaida Luiza".

"Najua bosi, usiwe na wasiwasi".

Ofisi ya Chifu haikuwa mbali sana na yangu kwani tulikuwa kwenye ghorofa moja. Nilipofika nilifungua mlango wa chumba cha Katibu wa Mkurugenzi wa upelelezi.

"Halo Maselina, hujambo".

"Sijambo, Willy siku hizi hatugongani?"

"Kazi nyingi, na vile vile wewe unaadimika kama shilingi ya mwambo!"

"Nhuu, usinitanie wewe ndiwe..." Kabla hajamaliza hiyo sentesi yake mlango wa Chifu ulifunguliwa na Chifu mwenyewe akatoa uso ulioonekana wa ukali sana.

"Waheshimiwa wamo ndani wanakusubiri wewe, na wewe unacheza hapa".

"Samahani Chifu", nilijibu kwa aibu.

"Maselina, hatutaki simu mpaka iwe ya lazima sana. Chifu alisema kwa sauti nzito.

Nilipoingia kwenye ofisi ya Chifu nilishangaa sana. Mimi nilitegemea huu kuwa moja ya mikutano yetu ya kawaida, lakini nilishangaa kuwaona Mkuu wa Polisi na maafisa wa kizungu ambao sikuwafahamu. Pamoja na hao walikuwepo maofisa kadhaa wa polisi. Kwenye meza ya mkutano kulikuwa kumebaki kiti kimoja ambacho nilihisi ni changu. Baada ya kuwasalimia wote nilienda nikaa kwenye kiti hicho.

"Nafikiri wote tunafahamiana?" Chifu aliuliza.

Wote tulitingisha vichwa.

"Nasikitika kukueleza kuwa huu si kama mikutano yetu ya kawaida, mkutano huu una jambo lake la pekee na ndiyo sababu unawaona maafisa hawa wageni wanaotoka katika Shirika la polisi Duniani (Interpol) Wote wamekuja kutusaidia kutatua matatizo ya uhalifu ambayo yanatushinda na ambayo kwa kweli yanahusu dunia nzima".

Nikaweka majalada yangu pembeni.

"Unamkumbuka Jack Mbwile?"

"Ndiyo namkumbuka. Nimewahi kufanya naye kazi, wakati nilipokuwa nimetumwa kwenye kazi moja huko Ziwa Tanganyika. Katika Idara yetu ya upelelezi ndiye alikuwa nambari moja katika kuogelea. Aliweza kuogelea kutoka Visiwa vya Unguja hadi pwani ya Tanzania Bara".

"Basi Jack amekutwa amekufa huko Mwanza kando kando ya Ziwa Victoria mahali paitwapo Mwanza South", Chifu alieleza.

"Loo! Alikuwa anafanya nini huko?" Nilimuuliza haraka.

"Marehemu miezi miwili iliyopita tulimshirikisha katika Idara ya Polisi kusaidia upelelezi wa wizi na uuzaji wa magendo ya almasi. Yapata miezi kama minne hivi tuliombwa na polisi kushughulikia jambo hili ambalo sasa lilikuwa limefikia kiwango kibaya, kwani ripoti iliyotoka kwenye machimbo ya almasi ya Mwadui inasema ya kwamba kwa muda wa miezi sita iliyopita madini yaliyo tayari kusafirishwa yamepungua kwa asilimia arobaini na tano kuliko kawaida. Hii haitokani na kupungua kwa madini, ila inatokana na wizi.

"Idara ya polisi imejishughulisha sana na upelelezi wa wizi huu, lakini wameweza kushika wezi wadogo wadogo ambao hawawezi kuleta tofauti yote hii. Kwa hiyo wametuomba msaada juu ya jambo hili. Papo hapo tulimtaka Jack akiwa huko

Mwanza atusaidie. Kwa bahati mbaya habari nilizozipata asubuhi hii ni kwamba Jack amekutwa amekufa. Polisi wameeleza kwamba amekufa maji. Upelelezi zaidi bado unaendelea juu ya kifo hiki. Mimi naamini kuwa Jack hakufa maji, atakuwa ameuawa na pengine amehusika na habari hizi za wizi wa almasi."

"Tokea aende Mwanza ni muda gani sasa?" Nilihoji.

"Yapata mwezi unusu".

"Alikuwa bado hajatoa ripoti yoyote?"

"Bado. Kwa jinsi mambo yalivyo ndiyo sababu Waziri pamoja na maafisa hawa wa Usalama wamefika hapa. Wamekuja kutafuta mbinu zaidi za kulitatua jambo hili. Waziri anaitaka Idara hii itoe msaada wa hali ya juu ili kulitatua jambo hili ambalo linagusa uchumi wa Taifa letu. Nimekuita hapa uelewe uzito wa jambo hili na uchukue dhima ya Taifa katika kupeleleza.

"Idara yetu imelipa tatizo hili nafasi ya mbele katika kazi zote na wewe utaziacha kazi zako zote zingine na kuchukua kazi hii. Utafanya kazi bega kwa bega na Polisi na kwa sababu wao wamekuwa wakishughulika na jambo hili kwa muda mrefu watakupa kila msaada wa maelezo yatakayokusaidia katika jambo hili. Tumekata shauri kukomesha kabisa wizi huu.

"Mpaka sasa kuna fununu ya watu fulani fulani ambao wamesambaa Afrika Mashariki nzima ambao wanaweza kuwa shina la tatizo hili. Lakini namna ya kuweza kuhakikisha na kuwatia mbaroni imekuwa inatushinda. Jambo ninalotaka kuongeza kidogo tu ni kwamba serikali inaamua kila njia ifanyike jambo hili likomeshwe. Kwa wakati huu ambao nchi yetu inahitaji pesa za kigeni sana, ni dhahiri kuwa serikali hairidhiki kuona jambo hili linaendelea. Kwa hiyo, kijana, umetwishwa mzigo mkubwa na nchi yako na ni imani yangu kuwa utafanikiwa. Hatutavumilia kuona watu wachache wanadhoofisha uchumi wa nchi nzima. Mungu akusaidie".

Maneno haya yalinichoma mno maini. Neno moja tu ndilo niliweza kujibu.

"Amina".

"Habari za maendeleo yako nitazipata kutoka kwa Mkurugenzi wako", Waziri alimalizia.

"Kama nikirudi hai", nilijibu huku nikitabasamu.

Tuliagana naye kisha mie nikaondoka.

Ofisini kwa katibu wa Chifu nilimkuta katibu wangu.

"Unafanya nini huku nami nimekwambia ukae ofisini?"

"Kuna mtu anakuhitaji kwa haraka eti ni mvuvi kutoka Mwanza".

"Mvuvi ananitafutia nini mimi?"

"Nitajuaje, yeye anasema ni lazima akuone".

Twende basi."

"Ndiyo hata kwaheri hamna?" Maselina alilalamika.

"Loo, kichwa changu kimevurugika, kwaheri, ngoja nikimbie. Chifu akifungua mlango na kuniona hapa tena atanifukuza kazi. Wote tulicheka na kuondoka. Tulipofika ofisini kwangu nilimkuta huyo aliyeitwa mvuvi amekaa kwenye viti vya wageni.

"Karibu ndani".

Akaingia.

"Keti chini".

"Asante".

"Habari za Mwanza".

"Nzuri tu".

"Nikusaidie nini?"

"Mimi naitwa Matayo Buluba, kazi yangu ni mvuvi". Kisha akatoa picha mfukoni mwake akanipa. Katika picha hiyoalionekana yeye akiwa na marehemu Jack Mbwile.

"Unamfahamu huyo?"

"Ndiyo, ni Jack Mbwile".

"Sawa, wewe ni Willy Gamba, siyo?"

"Ndiyo, umenifahamu wapi?"

"Ndugu huyu nasikitika kusema sasa ni marehemu!"

"Nimesikia".

Nilipojibu tu hivi akaonyesha sura ya kushangaa!.

"Nimepata habari, usijali nimejuaje, wewe endelea na maelezo yako.

"Marehemu tulionana yapata kama mwezi hivi, na alikuwa mtu mzuri sijapata kuona. Nilikuwa nakaa naye huko Kirumba. Tulionana siku moja Ziwani, na katika mazungumzo tukaelewana. Yeye alikuwa anapenda sana kuogelea na mimi ni mwogeleaji mashuhuri Mwanza . Tumewahi kufanya mashindano ya kuogelea na kwa mara mbili hivi ameshinda. Kisha katika mazungumzo na kutaka kujua anakaa wapi ndipo aliponieleza kuwa alikuwa amefika siku chache tu zilizopita na kwamba alifikia Hoteli ya Mwanza. Mwanza alijia shughuli za kibiashara.

"Wewe wakati huo ulikuwa unaishi wapi?"

"Nilikuwa naishi Kirumba, na nilikuwa naishi katika nyumba yangu mwenyewe, yenye vyumba vinne".

"Ulikuwa umeoa wakati huo?"

"Nilikuwa nimetaliki na nilikuwa bado sijazaa na huyo mke. Na kwa vile nilikuwa sina mpangaji nyumbani mwangu nikakata shauri Jack Mbwile aje tuketi wote, naye akakubali. Alikuwa mtu ambaye unaweza kumzoea mara moja tu".

Alinyamaza kidogo na kuniangalia. Alipoona sina la kusema akaendelea.

"Kila siku alikuwa anaodoka kufanya shughuli zake na miye nikienda zangu kwenye shghuli za uvuvi. Tukionana jioni alikuwa akinichukua na kwenda kutembea kidogo kwenye moja baridi moja moto". Alitabasamu kidogo kisha akaendelea. "Ila siku zingine alikuwa harudi mpaka asubuhi. Leo ni Ijumaa siyo?"

"Ndiyo".

"Sasa. Jumatatu tangu atoke asubuhi hakurudi mpaka tulipoonana Jumanne saa kumi wakati aliponifuata ziwani nilipokuwa nikisuka mitego yangu. Baada ya kusalimiana aliniomba niache kazi hiyo kidogo twende nyumbani. Tulipofika nyumbani aliniambia kuwa usiku wa Jumane hiyo alikuwa na mkutano mkubwa sana ila ulikuwa na hatari. Pia akanieleza kuwa jambo lolote likimpata nije Dar es Salaam. Aliniandikia jina la mtaa na jengo na nije nimuone mtu aitwaye Willy Gamba. Alisema kuwa nikimuonyesha huyo mtu picha tuliyopiga wote atanipokea vizuri kwani ni ndugu yake. Kisha alinipa na bahasha hii".

Alitoa hiyo bahasha na kunipa. Kisha akaendelea.

"Bahasha hii ilikuwa nikupe kama jambo limemtokea, kama angerudi angeichukua mwenyewe. aliniachia shilingi elfu moja za kusafiria ikibidi",

"Wewe ulimshauri nini?"

"Mimi nilimshauri asiende ikiwa ameona kuna hatari katika mkutano huo. Lakini aliniambia ni lazima aende kulikuwa na jambo la lazima sana katika mkutano huo. Nilimweleza kuwa ingefaa twende wote, lakini vile vile alikataa. Kisha tuliagana akaondoka. Usiku mzima sikulala kwa kumsubiri na hakurudi Jumatano yote hakuonekana, Usiku wa Jumatano pia sikuweza kulala.

"Jana mnamo saa nne hivi nilikwenda ziwani kuwangoja wavuvi wenzangu waliokuwa wamekwenda kuvua. Huko ndiko nilikopata habari hizi za huzuni. Wavuvi wa huko Mwanza South walinieleza kuwa wamemkuta rafiki yangu amekufa maji mnamo saa kumi na mbili na nusu asubuhi. Nilishangazwa sana nikakumbuka maneno yake. Badala ya kwenda polisi nikakata shauri kuja kwako moja kwa moja".

"Wavuvi walinieleza kuwa polisi walikuwa wameishachukua mwili na kuupeleka hospitali na upelelezi wa kifo umeanza. Saa nane nikakodi taksi na kuja huku, nimefika leo asubuhi." Alinyamaza huku machozi yakimtoka.

"Loo, jambo la kuhuzunisha sana! Huyu ni rafiki yangu sana. Asante sana kwa habari zote, mimi nitakuja Mwanza na nitakuja kukuona".

Niliandika taarifa yote na nikamshukru sana. Nilimpa kiasi cha fedha kumsaidia nauli na masumbufu ya njiani.

"Sawa, unatarajia kurudi lini?" nilimuuliza.

"Narudi leo kwa basi".

"Mimi nitafika kesho".

"Njoo kesho kutwa Kirumba Na. 32 ndiko nyumbani kwangu. Haya kwaheri, nataka nirudi mapema huenda Polisi wananitafuta".

"Wakati unafika Mwanza na mimi nitakuwa nimefika, usiseme lolote kwa polisi mpaka tumeonana. Vitu vyake unavyo?"

"Nimeviacha Mwanza. Akili yangu ilikuwa imevurugika kwa hiyo nilikuwa tu nataka nikuone kwanza ndipo roho yangu itulie".

"Basi viweke mpaka nifike. Kwaheri".

Tulishikana mikono tukaagana. Alipoondoka nikafungua hiyo bahasha, na ndani mlikuwa na karatasi kubwa lakini imeandikwa neno moja tu. ELUNGATA.

Niliinua simu kumuita Katibu Wangu.

"Luiza, njoo.

Luiza alikuja mara na kuuliza.

"Niende sasa? Saa saba unusu sasa ingawa nimechelewa naweza kuwabembeleza wakamtibu."

"Mimi sikukuita kukupa ruhusa ila kukueleza kuwa leo hatutoki kwa saa za kawaida, ipo kazi kubwa sana ambayo inanikabiri. Kuanzia kesho, huenda sitakuwa ofisini kwa muda usiojulikana kwa hivi utakuwa na muda mrefu wa kuweza kumaliza shughuli zako binafsi maana sitaacha kazi nyingi".

"Kumetokea nini?"

"Nitakueleza nitakaporudi, sasa hivi hata nikikueleza hutaelewa. Mtume tarishi akuletee chakula chochote utakacho, mimi aniletee soda moja na sambusa nne".

"Asante".

SURA YA PILI

Luiza aliondoka nilianza kupanga mawazo ya namna ya kulitatua tatizo hili nililokuwa limepewa. Akili yangu ilizunguka huku na huku kutafuta ufumbuzi, na kila wazo nililopata nililiandika mara. Niliandika na kufuta na kusahihisha mara kadhaa wa kadha. Hata hivyo mwishowe nilifikia wazo moja maalumu la kuzingatia.

"Soda yako hii".

Nilistuka.

"Asante binti, siku nikibadilishiwa katibu, mimi nitaacha kazi".

"Ahaa, ama kweli utaacha kwani ulimwengu wote katibu akufaae ni Luiza tu? Nafikiri mimi nitakuwa wa kwanza kuacha. hakuna msichana asiyenichukia hapa ofisini".

"Usijali. Sasa saa ngapi?"

"Saa tisa kasoro robo".

"Nitakuletea kazi baada ya dakika kumi na tano hivi. Kazi utakayopata jitahidi kuimaliza kabla ya saa tisa na nusu maana nina mkutano na Chifu saa kumi".

"Ama kweli leo iko kazi, kuna mkutano mwingine saa kumi?"

Alifungua mlango na kwenda ofisini kwake. Niliendelea kuanika mpango wangu kwa makini. Nilipofika hatua ya mwisho simu yangu ikalia.

"Hallo nani?" Niliuliza kwa ukali.

"Kuna bibi kwenye simu" Luiza alijibu kwa woga, maana alijua nimeudhika.

"Hallo nani?"

"Ndiyo saa nane na dakika thelathini na tano juu ya alama ya kikwenu hii! Una maana gani ya kuniweka mpaka dakika hii huku ukijua huji!" Didi alijidai kufoka katika simu.

"Didi mpenzi samahani sana. Nimepata kazi muhimu sana ya haraka sana hata nimeshindwa kutimiza ahadi yangu."

"Mimi najua hunijali hata kidogo, ungekuwa unanijali ungeweza hata kunipigia simu kunieleza yote hayo ili nisikungoje".

"Si hivyo Didi. Wewe wajua kabisa kuwa nakupenda sana. Ni kazi iliyonitinga hata nisipate wasaa wa kukuona. Hata hivyo nitafika, ningoje mnamo saa moja hivi, tafadhali kwaheri".

Nilikata simu kabla hajaaga. Hii kazi yangu inamfanya mtu kuwa kama mtumwa, hata wakikwambia baba yako kafa yakupasa umalize kazi kwanza ndipo uende kwenye kilio. Niliendelea na kazi na baada ya kumaliza nilimpelekea Luiza.

"Piga nakala tano".

Mnamo saa kumi na dakika tano niliingia ofisini kwa Chifu. Maselina alikuwa anapiga chapa.

"Wamo ndani?"

"Wamo wanakusubiri".

Nilifungua mlango na kuingia ndani. Niliwakuta Chifu, Mkuu wa Polisi na wageni wengine.

"Habari za mchana?" Niliwaamkia.

"Nzuri", walijibu kwa pamoja.

Niliwagawia nakala za mawazo yangu ya awali. Katika taarifa yangu hiyo kitu kilichosisitizwa ni misaada maalumu niliyohitaji na ushirikiano wao wakati nikifanya upelelezi. Wote waliafiki na nikaachwa niendelee na shughuli hiyo. Ilikuwa sasa yapata saa kumi na mbili nilipowaaga.

Chifu aliita nilipofika mlangoni.

"Gamba".

"Naam".

"Tafadhali ujihadhari sana", alisema kwa huzuni.

"Bila ya shaka".

Chifu alikuwa akinipenda sana na kila nilipokuwa nikienda safari za hatari roho yake huhuzunika mpaka nirudipo. Nilimkuta Maselina akisoma gazeti. Aliponiona akatabasamu.

"Vipi? Safari tena?"

"Ndiyo binti".

"Safari salama urudi na zawadi".

"Kama nikirudi".

"Bila ya shaka utarudi. Tutakuombea kwa mola".

"Kwaheri ya kuonana".

Nilipofika ofisini kwangu, nilimkuta Luiza anapiga simu.

"Vipi unapiga simu?"

"Nampigia rafiki yangu huko Kurasini".

"Sasa binti mimi sintakuweapo nitaondoka saa tano kwenda Mwanza kama ulivyoona kwenye ripoti. Shughuli za hapa shughulikia kama kawaida. Tatizo lolote peleka kwa Chifu".

"Unategemea kurudi lini?"

"Siwezi kujua, naweza kuchukua muda mrefu sana au mfupi sana. Na huenda nisirudi kabisa".

Akijidai kusikitika.

Ukisema hivyo basi utatufanya wenzio tukonde bure kwa wasiwasi".

Baada ya kuagana na Luiza nikaondoka kwenda kumuona Didi. Didi ni mpenzi wangu wa muda wa miezi sita akiishi katika ghorofa za huko Ilala. Ni mzuri kwa umbo na pia mawazo na mwenendo wetu unapatana. Amehitimu na kupata shahada ya digrii katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati huo alikuwa akifanyakazi katika Shirika la Bima la Taifa kama Afisa Maslahi na ulikuwa ndio mwaka wake wa kwanza wa kazi. Nilipofika huko nilisimamisha gari langu la kikazi nje, kisha nikapanda ngazi kwenda kwenye ghorofa yake kumbe Didi alikuwa ameniona nikija na kabla sijabisha alifungua mlango.

"Karibu, wa ubani."

"Asante".

"Ndiyo ukanifanyaje leo?"

"Haya basi yamekwisha!".

"Binti nasikitika kukueleza kuwa nitakwenda safari usiku huu. Na safari yenyewe ni ya kikazi na ya lazima."

"Safari zako haziishi mimi bado sijakaa nawe safari! Utajuaje mapendo yangu? Maneno yangu? Wasiwasi wangu! Mbona hivi Willy?"

"Tuliza roho yako ya Mungu mengi siku moja utapata muda mrefu mpaka utachoka."

"Nilikuwa na mambo ya kukueleza lakini sasa naona huna nafasi hata kidogo, ukirudi nitakueleza. Utarudi lini?"

"Inategemea na kazi itakapokwisha."

"Unaenda wapi?"

"Mwanza".

"Willy, nitapungukiwa na mtu! Sijui itakuwaje wakati huu ambao hutakuwapo. Mazoea kweli ni adhabu."

"Uwe na moyo mgumu, nitarudi karibuni."

"Nasikia wivu pia, huenda ukaonana na wasichana wengine huko."

"Huniamini, Didi? Unanisikitisha sana!"

"Si hivyo Willy, nakupenda mno ndiyo sababu nakuonea wivu."

Didi alinishika mkono na kunivuta na kunikumbatia. Damu yangu ilikimbia upesi upesi lakini nikajikaza roho na kumsukuma. Didi alikuwa ameng'ang'ania shingoni mwangu.

"Nenda binti, nitachelewa!"

"Haya baba kwaheri." Alisema na huku machozi yakimtoka.

"Hunitoi hata nje!"

"Hata"

Akilia.

Kwa uchungu nikatoka. Nikafunga mlango wake kwa nguvu nikaondoka. Nilikwenda kwanza kwa daktari anipe mahitaji yangu muhimu kwa kazi kubwa ya upelelezi wa wizi wa almasi.

Safari yangu ilikuwa safi sana. Nilitumia saa kumi na mbili tu mpaka Mwanza. Ilikuwa saa tano asubuhi nilipoingia Mwanza. Nilikwenda moja kwa moja hadi Hoteli ya Mwanza katika mtaa wa Posta. Niliegesha gari nje na kuchukua mizigo yangu madi Mapokezi ya wageni.

"Habari ya leo ndugu!"

"Nzuri, tukusaidie nini?"

"Naweza kupata chumba?"

"Bila shaka, vyumba vipo chungu nzima".

Alileta kitabu na kunipa.

"Jaza humo ndani".

Nikajaza Jina Mark Buhulula. Kazi Mfanyabiashara. Anuani S.L.P 3300 Shinyanga: muda wa kukaa siku kama kumi hivi. Nitokako Shinyanga, kwenda Mwanza, nikamaliza kujaza yote haya.

"Nitakupa chumba namba 230 ghorofa ya pili".

Kisha akamwita mtumishi mmoja.

"Juma njoo hapa".

Juma akafika.

"Mpeleke huyu ndugu chumba namba 230".

Juma akabeba mzigo wangu tukafuatana. Chumba kilikuwa kizuri sana.

"Unataka nini? Aliuliza.

"Hiyo ni asante yako".

"Loo asante sana ndugu. Ukitaka msaada wa aina yoyote ile niambie nitakusaidia".

"Ikibidi nitafanya hivyo".

Nilifungua mizigo yangu na kuiweka vizuri. Chupa aliyonipa Chifu niliifungua. Loo Mlikuwa na vipande vya almasi vinne vizuri sijapata kuona. Hata miye mwenyewe moyo wangu ulipiga haraka haraka. Hivi vipande vinne tu vingeweza kunifanya tajiri maisha yangu yote. Kisha nikapunguza mawazo yangu, nikavirudisha ndani ya chupa na kuviweka mahali pa usalama nikainua simu ya humo chumbani.

"Naweza kupata Dar es Salaam?"

"Namba gani?" Aliuliza Opereta wa kike kwenye simu.

"Dar es Salaam 08381".

"Nitakwita".

Nilijilaza kidogo kitandani. Zilipita dakika kama kumi hivi, kisha simu ikalia. Nikainyanyua haraka.

"09351 Dar es Salaam hapa, nikusaidie nini?"

"Willy hapa, hujambo Maselina?"

"Sijambo, vipi huko?"

"Niko MWanza Hoteli".

"Vizuri, nitakupigia simu baadae ndugu", akakata simu.

Nilionelea nioge kisha nipate chakula cha mchana, halafu nije nilale kidogo, maana nilikuwa bado sijalala. Baada ya chakula nilirudi chumbani na kulala. Niliamshwa na simu mnamo saa kumi hivi.

"Hallo nani?"

"Simu yako", alijibu opereta.

"Hallo Mark hapa".

"Subiri, zungumza na Chifu".

"Mark habari za saa hizi?"

"Nzuri, nilikuwa nimelala".

Mnamo saa moja hivi nenda forodhani, kuna boti moja inawasili toka Ukerewe. Ndani ya boti hiyo kuna mtu mmoja aitwaye Makungu Majula ana habari za maana sana ambazo huenda zikafumbua tatizo letu bila matatizo makubwa. Atakuwa amevaa jamba-koti moja la kaki na kofia nyeusi. Umwonapo nenda mpokee halafu taja neno Inter na yeye atajibu Inter halafu mtazungumza.

"Nitafanya hivyo, asante", nilijibu.

Nilipiga simu mapokezi kuwaomba wanileteee chupa moja ya Dimple pamoja na sprite kama tano hivi na barafu. Hiki kinywaji kingeweza kunisukuma hadi wakati wa kwenda forodhani kumpokea Makungu.

Mnamo saa kumi na mbili unusu niliondoka kuelekea ziwani. Mwendo wa kutoka Mwanza Hoteli mpaka forodhani ni kama dakika kumi tu hivi. Saa moja kasorobo ilinikuta tayari niko forodhani, kulikuwa na watu wengi ambao nao walikuwa wamekuja kuwalaki wageni wao. Nilipoangalia ziwani niliona boti ikija kwa mbali kidogo.

"Bana jambo?" Mhindi mmoja alinisalimia.

"Sijambo ndugu".

"Hii boti toka Kerewe? Mimi iko kuja goja toto yangu, toka kwa rafiki yake Nansio."

"Na mimi nasubiri rafiki yangu kutoka huko huko".

Boti sasa ilikuwa imekaribia mita mia tano hivi. Mara tu tukashtukia kishindo kikubwa mno, na watu wote kuanza kukimbia huku na huku. Mara hiyo boti ikashika moto na vipande kurushwa huku na huku. Watu wengi walikuwa bado na mshtuko na walikuwa hata bado hawajaelewa nini kimetokea. Polisi wanamaji waliingia mara moja ndani ya boti yao na kuelekea huko kwenye boti kuokoa maisha ya wote ambao walikuwa wangali hai. Mimi nilikata shauri kutulia na kuangalia mwisho wake.

"Toto yangu, toto yangu", huyo Mhindi aliyekuwa anazungumza nami alilia. Kisha akachomoka kuelekea ziwani. Bahati nilimwahi nikamshika.

"Tulia kwanza huoni watu wanashughulika kuokoa abiria waliopata ajali? Ukijitosa na wewe majini utakuwa umefanya nini".

"Toto yangu peke yake, kama iko kufa na mimi iko kufa tu potelea mbali Mungu iko".

Wakati huo Polisi wengi walikuwa wamefika na kusaidia kutuliza watu waliokuwa wamekuja kupokea wageni wao kwani vilio vilikuwa vimevuma kote forodhani-kwa jinsi boti ilivyokuwa imeteketea hata mimi niliamini kwamba hakuna mtu hata mmoja aliyekuwa amepona.

Mara moyo wangu ukashituka na kuanza kuhisi kuwa hii hakikuwa ajali. Ajali imetokea kwa sababu Majula alikuwa ndani ya boti na alikuwa na habari za maana

za kunieleza mdomo kwa mdomo. Kama mambo ni hayo basi tayari walikuwa wameishanijua.

Niliangaza macho huku na huku ili niweze kuona kama kuna mtu yeyote anayeniangalia. Nikakuta hakuna nilimtoroka huyo Mhindi aliyekuwa sasa amekaa chini huku akilia na kujiingiza katika kundi kubwa, ambalo lilikuwa limeshafika kushuhudia ajali hii mbaya.

Boti za polisi na mashua za wananchi zilikuwa bado zinaokota Maiti za abiria. Mara tuliona boti ya polisi ikija na mtu mmoja, ambaye walikuwa wamemlaza ndani ya boti. Walipofika ufukoni nilisogea kuangalia na nikaona ni msichana ambaye naye alikuwa abiria ndani ya boti ya ajali. Alikuwa bado hai. Polisi Inspekta aliyekuwa karibu yangu aliwauliza ndani ya boti, "Wangapi wamepona?"

"Mpaka sasa nafikiri ni huyu tu".

"Mfanyieni huduma ya kwanza".

"Ndiyo, Afande".

"Sajenti Kibonye?" Inspekta aliita.

"Afande".

"Rudisha watu nyuma, huyu mtu aweze kufanyiwa huduma. Tulianza kusukumwa huku na huku. Sura ya huyu msichana ilikuwa tayari kichwani mwangu. Sikuwa na haja ya kukaa zaidi, nikaonelea niondoke maana giza lilikuwa linazidi. Nilikata shauri kurudi moja kwa moja mpaka hotelini kwangu. Niliingia ndani ya chumba cha chakula kwa ajili ya mlo wa jioni.

"Habari za jioni?" nilimsalimia mmoja wa watumishi wa hapo ndani.

"Nzuri tu, sijui utakula nini?"

"Samaki wapo?"

"Wapo ngege, ningu na hata kambale wapo ukiwataka".

"Nipe ngege na viazi".

"Asante".

"Niletee na CocaCola".

Wakati nangoja chakula nikaanza kuwa na mawazo chungu nzima. Majula alikuwa ameishauawa. Bila shaka alifahamika kuwa angekuja kuleta habari ambazo

ningemtia mtu hatiani. Nilikua sijaelewa huyu Majula alikuwa anafanya kazi gani na wala uhusiano wake na kazi yetu nilikuwa sijui. Nikakata shauri kumuuliza Chifu.

"Mtu mmoja kafanya watu chungu nzima kufa, kweli binadamu ni katili, nilifikiri sana. Hawa watu walikuwa wameamua kuzima wasifahamike ili waweze kuendelea na shughuli zao za kudhorotesha uchumi wa nchi. Lakini siku za mwizi ni arobaini. Waswahili husema.

Bado nikiwa na mawazo mengi nililetewa chakula. Nilikula kwa kujilazimisha, maana chakula kilikuwa hakiendi kabisa. baada ya hapo nilipanda chumbani kwangu. Nilipofungua mlango na kuwasha taa, mara nikajua mliwahi kuwa na mtu. Sehemu yote ilikuwa imechunguzwa kifundi sana. Hakuna kitu hata kimoja kilichokuwa kimechukuliwa: Hii inathibitisha kuwa tayari waliwakuwa wameshanifahamu, kwa hiyo ilikuwa hatari kubwa sana kwangu. Nilifungua chumba changu nikatelemka chini. Nilienda moja kwa moja mpaka Posta ambako niliingia katika kibanda cha simu.

"Halo, Opereta, naomba Dar es Salaam nambari 07911."

"Nambari yako ngapi?"

"Nambari yangu ni Mwanza 0233".

"Subiri nitakuita".

Nilisubiri kiasi cha dakika tano hivi halafu simu ikaita.

"Halo, wewe ndiye uliyeita Dar es Salaam?"

"Ndiyo".

"Haya weka shilingi sita".

Nikaweka shilingi sita.

"Sasa zungumza".

"Halo, mzee yupo?"

"Ndiyo, yupo nani wewe?" Sauti nyororo ya kisichana iliuliza.

"Mwambie Mark"

"Halo kijana vipi?"

Sauti ya Chifu ilikuwa na mshtuko kidogo.

"Mambo si mazuri. Yule mtu wetu kapata ajali kabla sijaonana naye. Boti aliyokuwa akisafiri nayo nafikiri imetegewa bomu imelipuka na kupasuka ovyo ovyo. Watu wote wamekufa ila msichana mmoja tu. Mambo naona sasa yanaanza kufurahisha".

"Sasa unasemaje?"

Nilihisi kwamba yote niliyomwelezea hakuyajali.

"Mipango ya operesheni yote naigeuza. Nikijipeleka kama nilivyopanga basi najichimbia kaburi. Inanibidi sasa nijihadhari. Nitahitaji msaada fulani fulani zaidi kutoka ofisi kuu.

"Vizuri, endelea unavyoona ni sawa, maana opereshani yote iko mikononi mwako. Kila unachohitaji utapata, kwaheri".

"Kwaheri, asante".

Nilipomaliza kupiga simu nilionelea huu ndiyo muda wa kwenda kumuona Buluba. Nambari ya nyumba ilikuwa 32 Kirumba. Niliondoka moja kwa moja kwa miguu kuelekea Kirumba na huku mawazo yangu yakinizunguka sana. Nilitafuta hiyo nyumba kwa bidii sana lakini kwa sababu nambari zenyewe hazikuwa na mpango ilinibidi niulize. Nilikwenda kwenye duka moja la Mwarabu kuuliza.

"Habari ndugu".

"Nzuri".

"Nyumba nambari 32 inaweza kuwa wapi?"

"Nasunguka pande ile takuta nambari 32".

"Asante".

Nilifuata maelezo ya Mwarabu na mara moja nikaiona. Nilibisha hodi mlangoni lakini hakukuwa na jibu. Taa ilikuwa ikiwaka ndani. Nilizungusha kitasa mlango ukafunguka, kumbe ulikuwa wazi. Huenda alikuwa ameenda dukani, nikaingia nimsubiri.

SURA YA TATU

Nyumba ilikuwa na sebule nzuri yenye saa kubwa sana ukutani. Nayo ilionyesha saa moja usiku, wakati nilipokuwa naingia. Taa ya chumba cha karibu nayo ilikuwa inawaka. Katika hali hii nikafikiria huenda amejilaza kitandani na usingizi ukamzidi. Nikaamua nimwangalie humo chumbani.

Lo! Nilipofungua chumba nilipata tishio jingine Matayo Buluba alikuwa ananing'inia darini amekufa! Jasho lilinitoka. nikashikwa na bumbuwazi kubwa. Jack Mbwileamekufa, Majulanaye! Sasa Buluba.

Wakati nakata shauri kuondoka nikasikia mtu anafungua mlango wa sebuleni. Nilijibanza kwenye ukuta karibu na mlango wa chumba cha kulala.

"Lazima utakuwa umeangusha humo chumbani", sauti moja ilisema.

"Huenda, lakini sidhani", alijibu mwingine.

"Fanya haraka, tafuta haraka haraka, anaweza akaja mtu akatukuta humu," sauti ya kwanza ilionya.

"Hapa sebuleni hakuna. Lo, sijui nisipoiona hiyo karatasi nitakwenda wapi!"

Kumbe walikuwa wanatafuta karatasi. Mara moja nami nikatazama huku na huku nikakiona kijikaratasi chini ya uvungu wa kitanda. Mara mlango wa sebuleni ukafunguliwa. Pandikizi la mtu likaingia, lakini bado lilikuwa halijaniona. Macho yake yalienda moja kwa moja kwenye hicho kikaratasi chini ya uvungu. Alipotaka kuinama ili akiokote kufumba na kufumbua alikuwa amelala chini kwa vile nilimpiga teke la uso bila ya yeye kutegemea.

Bastola aliyokuwa ameshika ilimtoka mikononi nami nikaruka kasi kuikota na kumwelekezea mwenzake ambaye alikuwa amepigwa butwaa. Kwa wepesi wangu nilifyatua risasi na kumpiga mwenziwe mkono wa kulia ambao ulikuwa umeshikilia bastola. Nayo ikadondoka bila ya yeye kutaka. Mwenziwe alipojaribu kujitahidi kunyanyuka hakua na la kufanya isipokuwa kusalimu amri yangu sasa.

"Kwanini mmemuua Matayo?" Niliwauliza.

"Sijui", hilo pandikizi lilijibu kwa hofu.

Hasira zikanipanda huku nimeshikilia bastola.

"Naona tunataniana. Mumemuua rafiki yangu na halafu mnafanya masihara, mtanitambua sasa".

Kabla sijafanya chochote nikakikumbuka kile kikaratasi ambacho nilikuwa nacho mikononi. Huku nimeshikilia bastola tayari, nilikisoma hicho kikaratasi. Kiliandikwa.

Ndugu Busy, fika Songwe klabu kabla ya saa sita usiku bila ya kukosa. Ukikosa usije ukanilaumu. Lonely.

"Huyu Busy ni nani?" Nilimuuliza yule pandikizi.

"Simjui, Tom ndiye alikuwa akimjua. Mimi huwa namsikia tu".

"Mwongo, sema ukweli la sivyo utamfuata mwenzio sasa hivi".

Wakati huo mwenzake niliyempiga risasi alikuwa akitapatapa kwa maumivu ya mkono.

"Kweli mimi simjui ila namsikia tu, ndiye anafanya mipango yote ya magendo ya almasi yeye ni kama wakala na.

Kabla hajamaliza mlango ulifunguliwa. Mimi mara moja nikaruka upande kama umeme. Kisu kilichokuwa kimetumwa kuniua kwa bahati nikamwingia pandikizi kifuani na mtu aliyekitupa akakimbia. Nilipomwangalia pandikizi alikuwa ameanguka chini huku damu ikimtoka kasi kifuani. Hakuonyesha matumaini ya kuepa kifo iwapo angebakia muda mfupi ufuatao.

Ingawa nilijikaza sana lakini nilianza kuona mahali pale hapakuwa na usalama wowotw kwangu. niliamua mara moja kuwapiga wote risasi mbili na kuondoka upesi iwezenavyo kabla jeshi la maharamia halijanivamia. Kisha nikakimbilia nje ili nirudi hotelini nilikofikia.

Sijui ni muda gani nilitumia lakini nilikuwa nikienda kasi mno. Sikuwa na haja yoyote ya kutafuta gari. Nilifika hotelini huku nikitweta na kutoa jasho jingi. Nilipotulia kidogo nikaoga na kubadilisha mavazi. Niliongeza risasi zaidi za bastola yangu kwa vile nilijua sasa maadui zangu ni wengi mno na itanilazimu mara kwa mara kupambana bila ya kutegemea. Funguo za chumba nilizichukua kwani nilikuwa wasije wakajua ni wapi nalala.

Sehemu hii ya mji wa Mwanza kuna kampuni ambayo unaweza muda wowote kukodi gari na ukaliendesha mwenyewe. Nikafanya hivyo na nikaamua kwenda Songwa Club kadri ya hicho kikaratasi kilivyosema.

Songwa Club iko kilomita kama kumi kutoka Maganzo, ama ni kama kilomita nne kutoka njiapanda iendayo Mwadui.

Nilitaka kuwahi kabla ya saa sita. Niliingia ndani ya gari nikafunga mkanda tayari kwa kuendesha mwendo wa kasi sana. Mnamo saa tano na dakika ishirini nilikuwa nimefika kwenye njia panda ya kwenda Mwadui na Songwa, lakini sababu nilifikiria kwamba sitaweza kurudi na kulala Mwanza nilikata shauri kwenda Maganzo nikalipie mapema chumba cha kulala katika nyumba ya wageni.

Nilipoingia Maganzo nikazungukazunguka kidogo halafu nikakata shauri kupanga chumba katika nyumba na baa iliyokuwa ikiitwa MASWA. Nilipoingia hapo baa ilikuwa imejaa hivi hata nafasi ya kukaa haikupatikana ingawa nilikuwa na kiu sana ya bia nilijikaza nisitamani.

"Halo," nilimwita mwanamke mmoja wa baa.

"Unasemaje?".

"Nataka chumba cha kulala".

"Subiri".

Baada ya muda mfupi akarudi.

"Kipo chumba kimoja tu, kina vitanda viwili kwa shilingi sitini tu".

"Sawa tu".

"Haya kalipe pale kaunta kwa yule mama mnene. Una mzigo?"

"Ndiyo, ni mfuko mdogo tu".

"Lipa halafu nitakuonyesha mahali pa kulala".

Nililipa na huyo mama akanionyesha chumba.

"Vyumba vyetu vizuri sana. Vitanda havipigi kelele", alieleza kwa tabasamu.

"Safi sana".

"Wewe unatoka wapi?"

"Mwanza".

"Unashughuli hapa?"

"Bila ya shaka, mtu haendi mahali bila ya shughuli. Lakini nataka kwanza kwenda kumuona rafiki yangu katika Baa ya Bantu".

"Tutaonana ukirudi".

"Asante".

Baada ya kupata chumba nilikifunga nikaondoka na kuingia ndani ya gari. Nilipoingia Songwa Clab ilikuwa saa sita kasoro robo. Kulikuwa na watu wengi, lakini kulikuwa na nafasi. Sikutaka kukaa chini kwenye meza maana ningeonekana mgeni na ningeweza kufahamika upesi.

"Halo, nipe bia baridi", niliagiza.

Bia yangu ilikuja nikaendelea kunywa. Niliangaza macho kwa chati baa nzima ili niweze kumuona mtu ambaye ana hali ya kumsubiri mtu lakini sikuweza kufanikiwa. Ilikuwa inafika saa sita na bado sikuwa nimeona kitu.

"Wewe ni mgeni hapa siyo?" Mtu aliyekuwa karibu yangu aliniuliza.

"Si sana, kwanini unauliza?"

"Nyuso za hapa tunazijua, au umeletwa Mwanza kwa uhamisho?"

"Hapana, kwani wewe unafanya kazi Mwadui?"

"Hapana, mimi nafanya hapo Songwe Stesheni ya Reli."

"Mbona maelezo yako ni kama karibu kila mtu wa Mwadui unamfahamu?"

"Si hivyo, maafisa wengi wa Mwadui huja kunywa na kutembea huku, tuseme maafisa wote wa Kiafrika wenye magari. Kule Mwadui hakuna wanawake, lakini hapa na Maganzo ndiko kwenye soko la watoto wa kike.

"Umekaa hapa Songwa kwa muda gani?"

"Lo, miaka kumi na miwili sasa. Toka nimemaliza darasa la nane nikajiunga na Reli ya Afrika Mashariki. Baada ya kutoka kwenye shule yao huko Nairobi nikaletwa hapa kama karani wa stesheni na leo niko hapa naitwa kama Stesheni Masta. Kwa hiyo Songwa, Mwadui na Maganzo nazijua kama kiganja changu".

"Miaka kumi na miwili, kweli umekaa."

Niliagiza bia zingine mbili, moja kwa huyu mtu. Bia zilipokuja huyu mtu akanishukuru sana.

"Asante sana, hapa watu hawanunuliani bia. Asante sana".

"Usijali".

"Ulisema unaitwa nani?".

"Mimi naitwa Mark, na wewe?"

"Abdul".

"Umetokea wapi?"

"Mimi nakaa Mwanza".

"Aisee".

"Ilikuwa sasa saa sita na robo na kulikuwa hakuna mabadiliko ya hali.

"Wanafunga saa ngapi siku hizi?"

"Kwa kawaida ni saa sita lakini wakati mwingine mpaka lyamba

Mara simu ikaanza kulia hapo kaunta. Akaipokea mfanyakazi wa kaunta. Baada ya kuzungumza kidogo akaita.

"We Mwenentumba kamwite Mzee Reuben kule ndani simu yake toka Mwanza.

Nilijisikia moyo wangu unapiga haraka haraka. Muda si mrefu kabisa. Alizungumza kwa muda mfupi akaweka simu chini huku amekunja uso akarudi huko ndani.

Huyu sehemu yote hii huitwa Pweke. Ni mtu hatari sana kuna tetesi kuwa anafanya magendo ya almasi ya hali ya juu. Polisi inasemekana wanamtafuta wameshindwa. Na ukitaka kumjua sana maisha yako hayawi marefu sana. Ni tajiri sana ana malori sana huko Shinyanga, Maganzo, Dar es Salaam na Mwanza. Vile vile watu humwita Pweke kwa sababu ni mara chache unamwona katika kikundi cha watu wengine", alinieleza taratibu.

"Yeye hukaa wapi?"

"Anakaa Maganzo, Shinyanga, Mwanza na Dar es Salaam, huko kote anakaa ana majumba lakini mara nyingi yuko Maganzo.

"Huenda basi nimemwona Mwanza".

"Bila shaka," Abdul alijibu. Hali yake ilionekana ni ya kulewa. "Tena nasikia yeye huwa anatumia dawa kuingia na kutoka Mwadui kuchukua almasi", aliendelea kueleza.

"Watu toka Afrika Mashariki nzima wanaoshughulika na magendo ya almasi nasikia wanamfahamu sana. Lo, ngoja ninyamaze nisije nikasikika nasema juu yake, maana nasikia ana masikio zaidi ya serikali. Polisi wenyewe tu hawathubutu kumgusa".

Niliagiza pombe zingine.

"Lete pombe".

"Loo, hakika nimefurahi sana, kaka wewe ni mtu mkarimu sana. Bahati mbaya mwezi umeniendea vibaya, miye ningekualika uje tunywe tena kesho, lakini nilikuwa na shilingi ishirini tu na nimeshamaliza. Hawa watu wa hapa hawathubutu kukopesha hata sisi wanywaji wa kila siku".

"Usijali, siku nyingine utajaaliwa."

Maelezo ya Abdul yalikuwa yamenisaidia sana.

"Mtu huyu ni wa ajabu sana. Ana dawa zinazoweza kusababisha kifo ana kujua mtu yeyote anavyomuwaza", alinieleza. Polisi akimfuatafuata anaweza kupata ajali akafa, au akafukuzwa kazi. Huenda hivi ninavyosema anasikia."

"Hawezi. Mbona una woga hivi".

"Wewe siyo mwoga? Sema baya lolote juu yake hapa Maganzo kama hatutakusikia umekufa kesho asubuhi. Wanawake wote Maganzo anawajua. Inasemekana anawaajiri wampe habari za wageni wote wanaoingia. Yeye huwalipa ujira wa kuwaridhisha hivi kwamba wasieleze habari hizi kwa mtu yeyote, ila Reuben. Askari kanzu wote wanaokuja kupeleleza habari za hapa hufa. Nimekaa hapa miaka kumi na nimeshuhudia wakifa. Wanawake wote sehemu hii ni wapelelezi wake. Lolote utakalosema litafika kwake. Sisi tunamwogopa mno," alimalizia na kisha akanywa matone ya mwisho ya bia yake katika glasi.

"Kunywa nyingine".

"Hapana, nimelewa anaenda".

"Unakaa wapi?. Nitakupeleka."

"Usijali, nakaa hapo mbele kama kilomita mbili tu kuelekea njia panda, lakini kwanza napita kwa rafiki yangu hapo karibu.

"Haya kwaheri nikipata muda nitakuja nikuone hapo stesheni kesho.

"Bila ya shaka karibu. Mara kwa mara urafiki huanzia kwenye tungi".

"Na kweli, basi tutaonana kesho".

Tulipeana mikono Abdul akaondoka. Ilikuwa saa saba kasoro robo hivi nikaagiza bia nyingine ya haraka haraka nielekee zangu Maganzo. Niliyokuwa nimeyapata yalinitosha kabisa ilinibidi kuzicheuacheua habari hizi kulingana na kazi niliyopewa kuwafichua na kuwakamata maharamia wa magendo ya almasi.

Wakati namalizia bia yangu ya mwisho. Mzee Reuben kama anavyoitwa alitoka ndani akamuaga mfanyakazi wa kaunta. Akaondoka kwenda zake. Nilipogeuka nikaona watu wamebaki wachache sana na kwenye kaunta tulikuwa tumebaki wawili tu.

Nilimaliza bia yangu nikamuaga mfanyakazi wa kaunta. Nikaenda zangu. Reuben alikuwa keshakwenda, maana hakukuwa na gari hapo nje.

Mawazo yangu yalikuwa mengi sana juu ya Reuben, Busy na kundi lao, nilitia gari moto kuelekea Maganzo. Nilipokaribia njia panda kwa mbele niliona kitu kimelala barabarani. Kwanza nilifikiri kwamba ni mbwa amekanyagwa lakini niliposogea karibu nikaona ni mtu. Niliposegea karibu zaidi nywele zangu zikasimama. Ni Abdul! Nikafunga breki bastola yangu ndogo nikaibana kwenye kiganja nikiwa tayari kwa lolote. Nilitelemka kwenye gari. Nilipomfikia nilikuta bado hajakata roho. Moyo wake ulikuwa unagonga kasi. Alionekana kama mtu aliyepigwapigwa sana au kugogwa na gari. Sikuweza kuona damu mahali alipolala.

"Hapo hapo! Nyama we!" sauti ilisikika mara tu nilipoinama ili nimwinue.

"Huyu mtu anakufa, niacheni nimpeleke hospitali", niliwajibu kwa ghadhabu.

"Wewe je? Hujihurumii mwenyewe kwanza?"

"Mniue basi mnangoja nini?" niliwajibu kwa hasira.

Niliamini kwamba saa yangu nami ilikuwa imefika, kwa hiyo kuomboleza kusingenifaa. Ilikuwa kufa na kupona. Bila ya kukawia nilifyatua bastola yangu na risasi zikawapata wawili barabara. Mwenzao wa watatu akakimbia na hamsini zake. Ndipo nikapata nafasi ya kumnyanyua Abdul na kumweka garini.

Maharamia hao wawili walikuwa wakitweta chini - mmoja wao alikuwa na bastola nayo ilidondoka kando. Niliiokona sikuwa na haja ya kuwachunguza bali niliwaburura hadi kando ya barabara na kuwaacha wafe huko. Kama kuna mtu atakayewaona bahati yao kwani palikuwa na majani marefu sana.

Abdul alikuwa hajakata roho. Niling'oa gari kutoka hapo kuelekea Shinyanga umbali wa kilomita thelathini hivi. Nilienda kasi sana hadi hospitali.

"Ndugu, nimemleta mgonjwa mmoja mahututi ndani ya gari", nilimweleza muuguzi.

Yeye haraka haraka akisaidiwa na mfanyakazi mwenzake walichukua machela na kumbeba Abdul. Machela ilisukumwa mpaka kwenye chumba ambacho kilikuwa na daktari ambaye alionekana kama alikuwa akisinziasinzia.

"Vipi? Ajali ya gari?" Daktari aliuliza huku akisogea kwenye machela.

"Hapana nimemkuta amelala kwenye njia panda ya Mwadui na Shinyanga. Nikatoka garini nikakuta amepigwa na bado anapumua kwa hiyo nikakata shauri kumkimbiza hapa hospitalini haraka iwezekanavyo".

"Lydia tafadhali mpeleke chumba cha uchunguzi, tayarisha vifaa vyote haraka mimi najaza cheti chake".

Lydia na John walisukuma machela kuelekea kwenye hicho chumba.

"Unafikiri atapona?" Nilimuuliza daktari kama mtoto mdogo.

"Sijui, inategemea amepigwa kiasi gani. Ukifika asubuhi tutafahamu, kwani unamfahamu?"

"Hapana. Nimemwokota tu. Hata hivyo ni mgonjwa wangu sasa".

"Sawa, umepiga ripoti polisi?"

"Bado. Nilikuwa sina budi kwanza kumleta huku maana mtu mwenyewe taabani sana"

"Sawa, jina lako nani?"

"Mark Buhulula".

"Unakaa wapi?"

"Mwanza".

"Kabila".

"Msukuma".

"Wa wapi?"

"Ntuzu".

"Haya asante sana. Utakuwa hapa Shinyanga muda?"

"Hapana, niko Maganzo".

Daktari akamtupia jicho na kurudisha mara.

"Haya asante. Ukiweza kufika asubuhi tafadhali njoo unione nitakueleza hali ya mgonjwa wako. Mimi ninamaliza kazi saa tatu asubuhi".

"Nitajaribu kuwahi daktari".

"Haya kwaheri, asante sana".

"Kwaheri na nyinyi, asanteni sana".

Niliondoka moja kwa moja hadi Maganzo. Nilitaka kumpigia simu Chifu usiku huo, lakini nikata shauri nimpigie asubuhi. Mawazo ya visa vya usiku yalinisumbua sana. Nilifikiri kuu ya majambazi hawa pamoja na vifo vyote. Kule Abdul kunong'onezana nami tu tayari ilikuwa imeshafahamika kuwa amesema mambo mengi, na wakawa tayari kumwadhibu kiasi kile cha kumuua.

Ilionekana kweli kuwapo kwangu Maganzo kulifahamika na nilikwisha kuwa mashakani. Na lile jambazi lililokimbia huenda limepeleka habari za kufa wenzi wao kwa Pweke.

Nilipokuwa nakaribia Maganzo nikakumbuka maneno ya Abdul kwamba hilo jambazi Pweke limenunua wanawake wote wa mji kwa kuwafanya macho na masikio yake katika kupata habari zozote zile.

Maganzo ilikuwa tayari kimya. Mji mzima ulikuwa tayari umeshatulia sana. Mabaa yote yalikuwa yamefungwa kwa hiyo niliendesha moja kwa moja kuelekea Bantu. Nilipofika Bantu Bar nikaegesha gari langu vizuri nikaanza kufunga milango kama kawaida. Baada ya hapo nikatembea kuelekea mlango ambao nilikuwa nimeonyeshwa nipite nikikuta baa imefungwa. Huu mlango niliukuta wazi, nikaingia ndani.

Nilienda moja kwa moja mpaka kwenye mlango wa chumbani kwangu. Niliangalia vizuri kuona kama umewahi kufunguliwa, lakini haukuonyesha wasiwasi. Nilifungua mlango bastola mkononi na kuingia ndani. Nilipoingia tu nikasikia sauti.

"Karibu ndani ndugu. Funga mlango na uwashe taa. Usilelte matata, kama hutaki kiadhirika".

Kwa kuwa kulikuwa na giza sikujua huyo mtu alikuwa peke yake au wengi. Nilikata shauri nifanye kama nilivyoagizwa. Nilirudisha bastola yangu mfukoni. Nikarudisha mlango na kuusingika. Nikawasha taa.

Ndani mlikuwa na watu watano. Mmoja wao alikuwa ameshika bastola imara na imeelekezwa usoni kwangu. Nilipowaangalia vizuri hao wengine kumbe nao walikuwa na bastola, wameelekeza kwangu.

"Kaa chini ndugu, usiwe na wasiwasi. Tungetaka kukuua usingefanya lolote, ungekufa tu".

Kulikuwa na meza ndogo na kiti. Nikakivuta nikaketi.

"Abdul ana hali gani?"

"Sijui, nilimwacha bado amezirai".

Nikamwangalia vizuri huyu mtu aliyeniuliza. Alikuwa kijana mwenye umri wa miaka ishirini na mitano hivi. Alionekana jasiri sana.

"Mimi nakuona wewe ni mtu jasiri sana, na ingawa nimeamriwa kukuua, nimeonelea kwanza nikupe onyo kama kawaida yangu niwaonyavyo kwanza wote waingiliao mipango yetu. Wengi nimewaonya, hawakusikia na wote wamefifia duniani. Ningependa na wewe uwe kwenye kundi hilo, kwa hiyo nakuomba uondoke sasa hivi baada ya sisi kuondoka, urudi zako Dar es Salaam. Mambo yaliyokuleta tunayajua. Mark Buhulula, na una bahati sana. Sasa hivi ungekuwa ulimwengu wa marehemu. Usipoondoka sidhani hiyo bahati itaendelea. Tatizo unalotaka kulitatua ni gumu mno. Linataka jeshi zima na si mtu mmoja. Saa tisa na nusu uwe umeshaondoka hapa mjini la sivyo usilalamike yakikupata".

"Nikikataa kuondoka je?"

"Kama wewe una akili naamini utaondoka, lakini kama umechoka na maisha baki. Tuone kama jua ya kesho litakukuta hai. Yaliyompata Mathayo umesahau, kwaheri ya kuonana kama umesahau. Twendeni zetu".

"Kwaheri, nitafikiria".

Bila kunijibu huyo kijana aliondoka huku akifuatwa na watu wake. Alinishangaza sana kwa utulivu wake na akaniogopesha vile vile. Nilibana mlango nikazima taa. Nilikaa kwenye kitanda nikifikiri. Nilifikiri kutimka niende zangu Mwanza halafu Dar es Salaam, lakini nikakumbuka kwamba nimetumwa kuja kufanya kazi. Nilikuwa nimekuja kuinua uchumi wa wananchi. Kwa hiyo nilikuwa sina budi kujitoa mhanga kama wenzangu walivyokuwa wamejitoa mhanga waliotangulia kabla yangu.

Baada ya mafikira haya nilikata shauri nisiondoke na nikae nione kutatokea nini. Kuja kunitisha nilijua lazima na wao

wana wasiwasi. Hivyo nilichukua mfuko wangu nikavua nguo nikatengeneza kitanda kama vile mtu amelala. Nikavuta kiti nikaa karibu na mlango. Nilitoa bastola yangu tayari kwa matatizo yoyote. Nikasinzia kidogo kwa sababu ya uchovu.

Nilikuwa nimelala kama nusu saa hivi, niliposhtuka kuangalia saa yangu ilikuwa karibu saa kumi asubuhi. Kilichonishtua sikukijua ni nini.

SURA YA NNE

Baada ya kitambo kifupi nikaona mtu ananyemelea kitanda. Alivyoingia sijui. Alikuwa na kisu mkononi. na wakati huo huo kwenye kona nyingine ya chumba niliona mtu amesimama na bastola mkononi. Wakati huo walikuwa bado hawajaniona maana waliamini nimelala hapo kama kitanda kilivyokuwa kinadanganya. Hivyo mtu alipofika karibu na kitanda mahali alipofikiria ni kifua, akainua kisu. Wakati anatelemsha kuchoma nami nikaachia risasi kwanza kwa huyo aliyeshika bastola na kisha kwa huyo aliyeshika kisu. Kukawa patashika katika chumba. Kisha nikawasha taa. Aliyeshika bastola alitapatapa na alipomuona mwenzake akipiga makambi ya mwisho akahudhunika na kumsemesha.

"Haa Deus unakufa?"

"Na wewe je mbona hujihurumii", nilimkebehi.

Nilimsogelea nikamchoma na kisu chao wenyewe. Nilichukua kamba mfukoni mwangu nikamfunga.

"Mliingiaje humu?"

"Kwa kupitia hapo juu".

Nilipoangalia nikaona kuna kipande kimoja cha ubao kwenye pembe moja ya dari kilichokuwa kimekatwa na kurudishwa.

"Wakati gani mambo haya yalifanyika?"

"Kati ya saa saba na saa nane".

"Ndipo kundi lile lote lilipopita mara ya kwanza?"

"Ndiyo".

"Mbona nyinyi mlipoingia sikuwasikia?".

"Angalia hivyo viatu chini".

Nilipoangalia nikaona soli zake zimetengenezwa laini nene zenye kufanana na matakia ya paka au chui. Kwa bahati nzuri risasi haikumpiga pabaya ni mkono tu ulioumia, alitapatapa tu kwa sababu ya hofu. Na kwa hivyo niliamini hii ni nafasi ya kumtumia mmoja wao. Huyo mwingine hakuonyesha matumaini ya kuishi kwani risasi nyingi zilimchakaza kifua.

"Twende".

"Wapi unanipeleka? Siendi popote iwapo wataka kunia uniue tu".

"Usinicheleweshe".

"Nimesema uniue, siendi popote".

Hasira zikanipanda na nikampiga mkono huu uliolemaa na risasi. Akalia sana kwa uchungu. Kisha nikambeba mgongoni na kumweka garini. Nilimpekua kuona kama ana chochote cha kunidhuru, nikaona hana. Bastola yake nilikwisha ipora.

Niliwasha gari moto na kuelekea Shinyanga. Niliondoka kwa mwendo mdogo sana sababu ya mawazo mengi niliyokuwa nayo baada ya haya yote kutokea ilinishangaza kuona wakati wote wa patashika katika chumba hicho hakuna mpangaji wa vyumba vya jirani aliyejitokeza. Imekuwaje? Mbona niliambiwa vyumba vyote vimejaa wageni! Nyumba hii haina budi kuchunguzwa. Nilikumbuka pia maneno ya Abdul ya kwamba jambazi Pweke amenunua wanawake wote wa baa wapeleleze kila mgeni aingiaye.

Jambazi nililokuwa nimelibeba ndani ya gari lilikuwa limeishazirai na mkono wake kufura vibaya. Hata hivyo nilikuwa nalisukasuka mara kwa mara na likapata maumivu makali. Wakati huo ndiyo nilipata nafasi ya kulihoji maswali kadhaa. Niliendesha gari mpaka karibu na hospitali ya Kolandoto, lakini porini kwa kufuata njia waliyokuwa wakipita ng'ombe.

Niliegesha gari huko mbali na barabara, ilikuwa yapata saa kumi na nusu hivi usiku na ilinibidi nifanye haraka shughuli yangu watu wasije nikuta waendapo shambani mapema asubuhi. Nilimtoa huyu mtu kutoka ndani ya gari nikamweka kwenye majani, nikisaidiwa na mbalamwezi. Nilitoa aina ya dawa kali mfukoni mwangu nikaiweka kwenye pamba kidogo nikamwekea puani. Haikupita hata dakika akapiga chafya na kuzinduka.

"Niko wapi hapa. Tunafanya nini?"

"Tulia, wewe ulikuja kuniua Maganzo, sasa ni zamu yako. Tuko porini wawili tu, na leo utanikoma.

"Nilikwambia uniue mbona hujaniua? Hata ufanye nini sikwambii lolote wewe niue tu".

"Mimi sikuui ila kuniambia utaniambia tu. Vua suruali upesi".

"Nitavyaje na wewe umenifunga?"

Nilimsogelea nikamsukuma kwa nguvu, akaanguka chini. Nilichukua kamba nyingine nikamfunga miguu. Halafu nikaanza kumvua suruali haraka haraka.

"Unataka kunifanya nini we?"

"Tulia, Nikikwambia kwa ustaarabu hutaki, sasa utanitambua".

"Niue tu, maana hata ufanye nini sisemi lolote".

Baada ya kushusha suruali na chupi nikazishika korodani zake.

"Jina lako nani?"

"Nimekwambia sisemi, husikii? Niue tu kama ulivyomuua Deus".

Nilipoona hivi nikazishika vizuri korodani zake, nikazivuta na kuziminya kwa nguvu. Punde akapiga kelele.

"Aaaa, aaa, niache sitaki".

"Jina lako nani?"

"Nicodemas."

"Unamfanyia nani kazi?"

"Sijui?"

Hasira ilinipanda, maana alikuwa ananichelewesha. Nilichukua koleo nikavuta korodani moja sasa. Nikaiweka katikati ya koleo nikaanza kuibana.

"Aaa, aaa, aaa ngoja niseme, tafadhali niachie nitasema yote, aaa, aaa, aaa".

"Unamfanyia nani kazi?"

"Ole".

Ole ni nani?"

"Ni yule tuliyekuja naye kwako usiku".

"Yeye Ole anamfanyia nani kazi?"

"Pweke".

"Pweke ni nani?"

"Yeye sisi hatumuoni mara kwa mara ila tunajua tu kuwa ndiye anaongoza hili kundi".

"Ni yeye pekee yake?" Niliuliza huku nikibana kidogo koleo".

"Ee hapana siku moja nilimsikia anasema na Ole juu ya mzee alisema mzee amekasirika sana huko Dar es Salaam. Ni hayo tu".

Nikabana kidogo tena.

"Nafikiri huyo ndiye mkubwa, lakini ana wenzake Shinyanga, Arusha, Mwanza, Musoma, Nairobi na Kampala. Hawa tumewahi kuwaona wanapokuja kwenye mkutano na sisi huwa tunaizunguka kulinda nyumba wanamofanyia mikutano".

"Shughuli yenu kubwa ni nini?".

Alishtuka kidogo juu ya swali hili, kisha akajibu, "Hujui ni almasi bila shaka wizi wote mkubwa wa almasi toka Mwadui lazima uhusike na kundi letu".

"Je, umewahi mwenyewe kuiba?".

"Sijui kuiba mimi ni mlinzi na nimeajiriwa kuua tu wako wanajua wameajiriwa kuiba".

"Kama nani?".

Nikabana koleo.

"Sijui hata jina moja nasema kweli tafadhali nasema kweli nasikia tu wengi wanafanyakazi huku Mwadui lakini kweli aaaa sijui jina hata moja".

"Mnalipwa kiasi gani?"

"Aaaa nalipwa shilingi elfu kumi kwa mwezi"

"Elfu kumi wewe mlinzi tu?"

"Ndiyo, kama akina Ole nasikia wanalipwa shilingi elfu ishirini kwa mwezi".

"Kwa mbali niliona mtu anakuja nikamtwanga Nicodemus na kitako cha bastola kisha nikambeba hadi garini, nikatia gari moto kabla huyu mtu hajatufikia. Nilipofika barabara kuu nikakata shauri nielekee Shinyanga. Ilikuwa yapata saa kumi na moja ya asubuhi sasa nilikwishajua kwamba ni wakati wa mapambano na kundi ambalo limejiandaa hasa na lenye kufurahia kazi yake kwa sababu ya ujira mkubwa bila shaka wana nidhamu kubwa. Ole na wenzie walijuaje kuja kwangu kabla hata sijaondoka Dar es Salaam watu waliojua ni Chifu, Mkuu wa Polisi,

Maselina, Lwiza, George na Didi. Lakini Didi hakuniona jinsi nilivyovaa au kuonekana wakati naondoka na wala hakujua jina langu lilikuwa Mark Buhulula. Nikakata shauri kupiga simu Dar es Salaam nijue kama kulikuwa na mtu mwingine aliyejua ambaye angeweza kuwajulisha juu yangu bila ya kujua yote haya. Ingekuwa vigumu sana kunitambua baada tu ya kuingia Mwanza.

Wakati nikifikiria hivi nikawa naingia Shinyanga mjini. Niliendesha moja kwa moja mpaka kituo cha usalama Shinyanga ambako nilimkuta askari wa zamu.

"Mkuu wa kituo yupo?" Nilimuuliza.

"Yupo".

"Naomba kumuona".

"Wewe nani na shida yako nini?"

"Nina mtu ndani ya gari mahututi, hivi tunavyozidi kubishana akifa mimi simo">

Nilipomwambia hivi akagutuka na kuchukua simu na kupiga.

"Mzee kuna mtu anataka kukuona... Sijui hajaniambia lolote" Kisha akanigeukia, "Nenda chumba nambari sita".

"ASante, angalia hiyo gari asitoke mtu au weka mlinzi kabisa shauri yako akikimbia". Kabla hajajibu mimi nikaelekea chumba namba sita. Nilibisha na kuingia ndani. Mkuu wa kituo kwa kufuatana na mavazi na tepe alizovaa alikuwa na cheo cha Inspekta.

"Habari Inspekta?"

"Salama, nikusaidie nini?"

Nilishika mfukoni mwangu nikatoa kitambulisho changu aliposoma akatoa macho ya woga huku akisimama kidogo alibabaika aseme nini.

"Nikusaidie nini mzee?"

"Nina mtu kwenye gari sasa amezirai lakini kwa muda tu wekeni rumande mpaka atakapopata maagizo zaidi na angalia asitoroke. Akitoroka bahati yako mbaya, utajua wewe mwenyewe. Habari hii isielezwe kwa mtu yeyote iwe siri yako mpaka hapo baadaye. Kwaheri, tutaonana tena ikibidi.

"Bila ya shaka mzee, mimi mwenyewe nitahakikisha maagizo yako yatatekelezwa," alisema huku akiondoka kunisindikiza.

Tulipofika kaunta akamwambia askari wa zamu. "Nenda ukamtoe mtu ndani ya hilo gari, mlete chumbani kwangu".

Baada ya kumtoa nikaingia ndani ya gari na kuondoka, nilitafuta mahali pazuri nikaegesha gari ili nilale kidogo. Nilipoamka ilikuwa saa mbili kamili, niliinua kiti cha gari nikawasha gari kuelekea kituo cha petroli. Baada ya kuweka mafuta nilikata shauri niende Hoteli ya Shinyanga nikapate kifungua kinywa. Nilipoingia hotelini nikaelekea msalani ambako nilikuta beseni. Nilipiga mswaki na kunawa sawasawa. Kisha nikarudi hotelini nikatafuta meza nikakaa. Mfanyakazi wa hoteli akanijia.

"Utakula nini mzee?".

"Nipe kahawa, mayai mawili ya kukaanga na maziwa.

Nikakaa kungoja chakula. Chakula kilipokuwa tayari kikaletwa nikaanza kula. Wakati nilipokuwa karibu kumaliza kula, nikashtuka watu wawili wanavuta viti na kukaa katika meza hiyo hiyo. Nilipoinua macho kuwaangalia nikatambua kuwa mmoja ni Ole na mwingine ni kati ya hao watu wake. Kijasho chembamba nikakihisi kutekenya maungo.

"Chakula chako kimeshalipiwa, inuka taratibu twende la sivyo angalia ubavuni".

Nilipoangalia ubavuni ndani ya kila koti la kila mmoja walikuwa washikilia bastola zenye viwambo vya kuziba sauti.

"Ok", nilijibu.

Nikaweka uma na kisu chinim, nikachukua kitambaa, nikajifuta.

"Hakuna ujanja, hatutaki kuua mbele ya watu, lakini ukitulazimisha tutafanya hivyo", nikaacha kitambaa changu na funguo moja juu ya meza nikainuka, wakanitanguliza huyo kijana aliyekuwa ameniletea chakula akanisemesha.

"Mzee, rafiki zako wameshalipa, asante sana".

"Asante kijana".

Mbele usawa na mlango nikamuona mtu wa tatu, nae mara moja nikaona kitu kinatokeza, nikajua alikuwa na bastola na nje kama mita kumi kutoka kwenye gari langu nikaona kuna gari aina ya Benz na watu wawili mara moja nikajua ndilo gari walilokuja nalo nilipokuwa usawa na huyo mtu wa tatu mlangoni, na huku hawa wawili wakiwa nyuma, kijana wa hoteli akaita.

"Mzee kitambaa umesahau".

Wote wakashituka na kugeuka hapo hapo nikapata nafasi kufumba na kufumbua ngumi mbili za nguvu kushoto na kulia shingoni mwa hao wawili wa nyuma yangu na wakati huo huo nikamtandika teke la tumbo watatu wote chini na bastola zao kabla hawajaamka mimi nilitimka na kurukia ndani ya gari langu wakati naweka gia ya kwanza ndipo Ole akaamka na kupiga risasi na huku mimi naondoka kasi risasi zake zote zilinikosa wakati naweka gia ya pili halafu ya tatu, nikamuona anarukia ndani ya hiyo Benz yao iliyokuwa na watu wawili wakanifukuza wawili waliachwa nyuma kwa hiyo gari likawa na watu watatu tulifukuzana barabarani na wakati nafika gereji moja katikati ya mji likatokea lori kubwa likakata barabara nzima nikakanyaga breki mara moja nikarudi gia namba moja nikazungusha usukani nikaweza kupita nyuma yake kabla halijanibana. nilipoona ninaweza kupita likaendelea mbele kuipa Benz nafasi.

Nilijaribu kuongeza moto zaidi, mara kukatokea trekta ambalo sikuweza kulikwepa, lakini nilipata kuruka kabla gari halijagongwa na kwisha kabisa nikaanza kukimbia nao walionifuata waliponiona wakatoka ndani ya gari na kuanza kunifukuza bastola mkononi huku Benz nayo ikikatisha kunifuata.

Nilikimbia mpaka kwenye jumba la shirika la usagaji ndani ya ghala la magunia ya mahindi ambayo hayajasagwa nilipandia dirishani na kujibwaga chini karibu na mlinzi nilimpiga ngumi ya shingo ili nipenye kumbe walikuwa wameniona nao wakaingia hapo hapo dirishani mimi nilijificha kwenye magunia nilipotulia ndipo nikasikia sauti zingine za wananchi zikisema, "mwizi mwizi mwizi".

Tulianza kutafutana kwenye magunia, nikamsikia mmoja karibu yangu akijisemea, "Yuko wapi?" Alikuwa karibu sana nami, nilipomwangalia yeye alikuwa bado hajaniona nikafundua kwamba ndiye yule aliyekuwa dereva ya hiyo gari alikuwa ameliacha nje, nilimpiga karate moja ya shingo na kumshindilia katikati ya magunia nilipompokonya bastoka yake na haraka haraka nikaelekea dirishani kusudi niwahi gari lao, nilipokuwa naruka dirishani wakaniona lakini risasi zilikuwa zimechelewa wakaanza kunifuata kupitia hapo hapo dirishani.

Nilipofika nje, bastola mkoni, nikaangaza huku na huku Benz lao lilikuwa na watu wawili ndani mara karibu yangu nikaona gari moja lenye msichana mmoja wa Kihindi naye anataka kuwasha nililikimbilia bastola mkononi nikapitia upande wa dereva nikafungua mlango na kumwekea bastola sikioni pale na huku nikimsukuma kwenye kiti cha abiria.

"Wewe sogea huko tafadhali".

"We fanya nini mimi pana kosa wewe miji".

"Sogea nitakueleza baadaye".

Majambazi yakatuona yakatupa risasi zikaipiga gari nayo ikayumba mimi nilishikilia usukani bila ya wasiwasi nikamuonya huyo msichana wa Kihindi.

"Wewe lala chini utauawa".

"Mungu mimi nafanya nini wewe, ua mimi pama kosa".

Nikaanza kukimbiza gari huku nakwepa magari na risasi huyu msichana wa Kihindi aliponiona ninavyoendesha akashangaa sana akainuka na kuangalia.

"Lala chini wanatutupia risasi, watakuua".

"Wewe fanya nini, ile natupa risasi ni polisi?"

"Siyo polisi wewe tulia nitakueleza".

Sasa walikuwa wanalikaribia saana hili haliwezi kupambana na Benz lakini nilijitahidi mbele nikaona kivuko cha reli karibu na daraja la kidaru. Na wakati huo huo nikaona gari moshi linakaribia saana kukata barabara kusimama ilikuwa haiwezekani. Maana Ole na wenzake wangenimaliza nikapata wazo.

"Fungua mlango na uwe tayari kwa kuruka, mimi nikisema tutaruka wote nitafanya maarifa usiumie".

"Wewe gari moshi itaua sisi ona iko karibu, aa bana simama sisi kufa".

"Fungua mlango, nasema shika maagizo yangu".

Aliponiangalia usoni akafuata maagizo, tulipogusa reli tu na gari moshi likagusa barabara.

"Sasa".

"Gari langu waka moto", alisema huku akilia huyo msichana wa Kihindi.

Tulikuwa tumeweza kuruka na kuangukia kwenye mtaro mrefu kiasi. Tuliona kwa juu moshi unatoka, nilipochungulia nikaona gari linawaka moto wa ajabu na watu wanakimbia ovyo kwenda kuangalia.

"Inuka twende, sitaki mtu atuone".

"Enda wapi?"

"Nyumbani kwenu, nataka kwenda kulipa gari lako".

Aliniangalia kwa mshangao mkubwa.

"Utaweza?"

"Wewe twende".

Wakati tunainuka watu wengi walikuwa wameishajaa hapo na nikasikia gari la wazimamoto linapiga kelele. Hii ilitupa muda mzuri wa kuondoka bila ya kuonekana.

"Wewe pana fuata mimi, mimi onyesha wewe jumbani yetu halafu wewe iko kuja".

"Nyumba iko wapi?"

"Wewe jua Butiama Hoteli?"

"Ndiyo".

"Jumba ya pili yake. Mimi tangulia wewe takuta nasubiri pana toroka kaka taua mimi, kama wewe iko toroka".

"Nitawasili, lazima nitakuja".

"Wewe mtu ya ajabu sana. Haya mimi nangulia ee".

"Haya".

Alitangulia akaenda zake. Mimi nikazubaazubaa hapo kidogo.

"Vipi pana nini pale mbona watu wengi?" Nilimuuliza kijana mmoja aliyekuwa anatoka kwenye hiyo ajali.

"Loo, afadhali ukajionee mwenyewe. Lo, ama kweli watu wengine wanakufa kifo kibaya sana. Gari moshi limegongana na gari dogo . Hilo gari dogo limevutwa likasagwasagwa na linaungua vibaya sana. Nasikia kulikuwamo mtu mwanamke mmoja wote wamekufa humo na vile gari lile linavyoungua hata mfupa hawauoni".

"Lo, hii ni ajali kweli. Watu wengine wana bahati mbaya kweli. Mtu mwingine anasema huyo mtu alikuwa jambazi anafukuzwa na askari kanzu lakini alipogonga tu na kuona amekufa lile gari la askari kanzu likakata kona na kukimbia. Nafikiri hao wanaogopa kuulizwa maana siku hizi siyo kama siku za ukoloni bwana".

"Walikuwa askari kweli?"

"Ndiyo mtu mmoja alivyokuwa anasema. Sijui kama ni kweli. Anasema magari yalikuwa yanakwenda mbio kweli. Nenda ukajionee mwenyewe".

"Asante", nilimshukru na kuondokana naye.

Kumbe Ole na wenzake walikuwa wanafikiri nimekufa? Hiyo ilinipa nafasi nzuri sasa ya kuwashtusha.

Niliondoka hapo nilipokuwa nimesimama na kuelekea kwa yule msichana wa Kihindi. Nilimkuta ameegemea mlangoni.

"Karibu".

"Ahsante".

"Hii ndiyo mtu nasema. Hii ndiyo kaka yangu Patel Jalali. Mimi kwisha sema kila kitu", alinijulisha kwa nduguye.

"Habari yako?", nilimsalimu.

"Juli, iko", alijibu kwa shingo upande huku amevimba kweli kweli.

Niliingia ndani nikasimama.

"Joo ndani sisi jungumja", alisema msichana huyu.

Tuliongozana wote watatu tukamuacha mfanyakazi wa Kiafrika dukani. Tulipoingia sebuleni tukakaa.

"We nani? Ni wewe fanya! Sisi taka ita polisi lakini Jasmini iko nakataa nasema kwanza wewe kuja halafu eleza".

"Mimi naitwa Willy Gamba." Nilitoa kitambulisho changu na kumpatia, aliposoma tu alipigwa na bumbuazi.

"Mjee basi sisi hapana sumbua wewe sahau," alisema huku akitetemeka na kumuonyesha kitambulisho Jasmini.

Jasmini alipokiangalia naye akashtuka.

"Sasa sikilizeni. Kaeni kimya, msizungumze na mtu yeyote juu ya habari hii. Mkizungumza mtajua nini kitawapata. Gari mlinunua shilingi ngapi?"

"Hapana hapana lipa. Sisi iko nasaidia serikali, sisi iko furahi tu. Sisi nyamaza kimya hapana sema hata neno moja".

"Lazima ilipwe, Jasmini sema shilingi ngapi?" niliuliza kwa msisitizo huku natabasamu.

"Zaidi ya elfu thelathini".

"Safi, nipe simu".

Waliponisogezea simu nikapiga Dar es Salaam kwa Chifu, wakati nangoja simu Patel akaenda dukani.

"Wewe taondoka leo?" Jasmini aliniuliza.

"Ndiyo".

"Hapana usiondoke, wewe mtu shujaa. Wewe kaa kidogo hapa", alisema na huku akitaka kulia.

"Lazima niende Mwanza, kazi bado".

"Baba yetu iko Mwanza, mimi nitakuja huko. Wapi mimi ona wewe? Mimi ondoka leo hii hii wewe wakati iko ondoka".

Nilipoona kubishana naye ni kazi bure nikafichua.

"Mwanza Hoteli".

Akatabasamu. Wakati huo huo simu ikalia.

"Hallo wapi hapo Willy?"

"Ulijuaje ni mimi?"

"Nilibuni".

"Nipe Chifu".

"Subiri".

"Hallo, hallo Mark, habari za huko? Nilikuwa na wasiwasi".

"Si nzuri kwani kuna malipo. Tengeneza hundi ya shilingi elfu thelathini kwa jina la Jasmini Halal S.L.P 12 Shinyanga utume haraka.

Nilinyoosha mkono Jasmini aondoke, akaondoka.

"Lo, na wewe kwa kuhonga pesa zote hizo kwa bibi. Pesa za serikali tena kwa bibi wa Kihindi," alisema kiutani. Kisha nikaanza kumweleza habari yote mpaka dakika hiyo.

"Lo, kweli kuna kazi kubwa. Jana baada ya mkutano tu Mkuu wa Polisi na Waziri wa Mambo ya Ndani waliitwa kwenda Lusaka, Zambia kuhudhuria mkutano. Kwa hiyo mambo yote ya polisi amekabidhiwa Kamishna Mkuu wa Polisi ambaye ndiye Kaimu wake." alinielza.

"Kwa hiyo toka jana habari zote anazo".

"Ndiyo".

"Nipe namba zake za simu".

"Jina lake ni Oswald Mengi. Si unamfahamu?"

"Ndiyo, nimewahi kumuona wakati wa kesi moja".

"Nimemtuma George toka asubuhi na mapema, nafikiri tayari yuko Mwanza".

"Asante sana".

"Haya asante, kazana Mungu atakusaidia tu. Hapo ulipofikia hakuna hata mtu aliyewahi kupafika. Asante kwaheri."

SURA YA TANO

Niliweka simu chini. Roho yangu ilifurahi kusikia George anakuja maana kazi ya wawili ni wawili. George alikuwa mtu wa nne kutoka kwangu, lakini nilikuwa nimemwamini sana. Ikiwa Sammy hayupo nilipendelea yeye kuliko Patrick ambaye ni wa juu yake. Alikuwa bado kijana sana, kijana mwenye umri wa miaka ishirini na mitatu. Lakini kwa hudo na karate hata mimi nilikuwa simfikii. Hivi alifaa sana kwenye misukosuko kama hii. Niliinuka nikamwita Jasmini.

"Mimi nakwenda".

"Haya sisi onana Mwanza jioni. Sawa bila shaka. Chunga ee, pana ile jangiri ua wewe".

"Nitajichunga".

"Kwaheri ee".

"Oke".

Nilimuaga Patel nikaondoka kwenda zangu. Ilikuwa saa sita hivi. Kwa vile gari langu lilikuwa limegongwa ilinibidi nitafute njia ya kwenda Mwanza ambako ningepata gari jingine. Nilikuwa sina njia bali kupanda gari la abiria au kuomba msaada kwa watu wenye magari waendao Mwanza. Wakati bado ningali katika fikra hizo nikaona gari linakuja na wazungu wawili, mwanamume na mwanamke. Nikawasimamisha.

"Naomba msaada gari langu limeharibika nakwenda Mwanza".

"Twende, sisi tunakwenda Musoma".

"Asante sana".

Niliingia akaweka gari moto".

"Wewe unakaa Mwanza?"

"Hapana, Dar es Salaam".

"Sisi tunakaa Musoma. Tunakaa Bukiroba Mision. Sisi tunaeneza habari za Mungu. Wewe ni Mksto?"

"Ndiyo".

Dini gani?"

"Protestanti".

Tulipovuka tu Shinyanga akalichochea moto gari.

"Lazima tuwe Mwanza kabla ya saa nane, tunamuwahi mtu", alieleza huyo mzungu mwanamume.

"Safi, mbona kiswahili chako kizuri sana?"

"Aaa. Lazima mimi nimekaa hapa nchini miaka zaidi ya thelathini.

"Ama kweli".

Kwa vile nilikuwa nimechoka sana nilijiweka vizuri nikasinzia.

"Amka tumefika", alinishtua huyo mzungu.

Nilipofumbua macho nikaona kweli tumefika Mwanza, tena mbele ya Mwanza Hoteli.

"Sisi tutakaa hapa," walinieleza.

"Mimi nimepanga hapa pia".

"Tumekuleta mpaka nyumbani. Hivi hatuulizani majina. Wewe ni nani?"

"Mimi naitwa Mark Buhulula".

"Ala, kutoka Ntuzu?"

"Ndiyo"

"Sisi ni Bwana na Bibi Jackson Filton toka Marekani.

"Nimefurahi sana mmenisaidia".

"Si kitu. Yesu anasema ukimsaidia mtu mwenye shida umemsaidia yeye, kwa hiyo ni wajibu".

"Asante, kwaherini".

Tuliagana.

Nilikata shauri kwenda chumbani kwangu nikapige simu ili nipate gari jingine. Wakati napita sehemu ya baa nikamwona msichana lakini sikukumbuka nilimuona wapi. Alikuwa msichana mzuri sana, mwembamba lakini mwenye siha. Nilikuwa

nimekwishamuona lakini wapi ndiyo nilikuwa nimeshindwa kukumbuka. Nilikata shauri nipande chumbani nipige simu halafu nirudi upesi huenda kwa bahati ningepata habari wapi nimemuona.

Wakati ninapanda nilipokaribia chumba changu nikapata fikra ghafla kichwani. Niliweka bastola yangu taratibu nikanyemelea chumba changu. Nilitazama huku na huku kama kuna mtu lakini sikuona mtu. Nilipokuwa karibu sana na chumba nikasikia sauti zinazungumza ndani na watu wanacheka. Niliposikiliza kwa makini nikasikia mtu anasema. "Sijui kaziweka wapi?"

Na mwingine akasema. "Tukipata hii mali ya serikali kweli mimi nitawacheka kweli kweli. Walete almasi yenye thamani kubwa nanma hiyo iporwe. Willy Gamba kesha kufa na sasa huko Delux na George naye atakuwa ameisha kufa, ama kweli mwaka huu serikali itatukoma.

Niliposikia habari za George gadhabu ikanipanda, bastola mkononi nikarudi nyuma kidogo na kwenda kimgongo mgongo kwa nguvu zote hadi kuugonga mlango. Mlango ulikuwa wazi hivyo nikaangukia ndani. Nao walishtuka mno wasijue la kufanya ghafla. Wakati huo huo nikawawahi watu wawili kwa risasi na kukawa patashika na hao ambao niliwakosa. Mmoja aliupiga mkono wangu kwa teke nayo bastola ikaponyoka, akanitwanga konde la haja. Hii inaniongezea hasira yangu vibaya sana.

Kabla sijasimama sawasawa akanitia teke la ubavuni mpaka chini. Aliponirukia nikamkwepa, Hapo nikajua kwamba kweli nimepambana na mtu na ilinibidi sasa niamue kupambana sawasawa.

Alitupa shoto lake nikalikwepa na hapohapo nikalishika hilo shoto na kwa njia ya judo nikamwinua juu na kumtupa chini. Aliposimama tu nikampiga karate mpaka chini. Nikamngojea tena asimame. Kumbe yeye alikuwa ameona bastola imedondoka karibu yake. Akaichukua, lakini kabla hajafyatua nikampiga teke.

Aliposimama tena alitupa ngumi nyingine. Nikaihepa na hapo hapo huo mkono wake wa kulia nikaupiga karate ukavunjika. Ulipovunjika nikamtwanga tena ngumi ya shingoni akaanguka chini taabani. Wengine walikuwa wamekimbia kasoro hao wawili niliowapata kwa risasi. Alipozirai nikamvuta mpaka kwenye bafu nikammwagia maji. Alipozinduka nikaushika huo mkono wake uliovunjika nikaanza kumuuliza.

"Nani amemfuata George?"

"Sijui", alijibu pole pole.

Nikaupinda huo mkono akasikia maumivu makali.

"Ole na watu wengine wanne".

"Mmejuaje amekuja?"

Nikaupinda tena huo mkono.

"Ole ndiye aliyekuwa na habari zote na pia ndiye aliyetuambia kuwa wewe umekufa".

"Mlikuja kufanya nini humu? Nani aliwaeleza nilikuja na almasi?"

"Ole".

"Nani aliyewaambia mimi ni Willy Gamba?"

"Ole".

Nilichukua kitako cha bunduki niliyoikuta humo ndani, nikamtwanga huyu mtu na kuhakikisha kuwa hataweza kuamka bila ya msaada. Halafu nikachukua bastola mbili nikazijaza risasi nikafunga mlango. Hapo chini nilimtafuta yule msichana yule mrembo lakini alikuwa ametoweka. Nikataka shauri kukodi teksi inipeleke kwenye Hoteli ya Delux.

"Kuna nini?" Dereva aliniuliza.

"Wewe nipeleke haraka iwezekanavyo".

Hakuuliza tena. Akawasha gari na kuondoka kasi. Baada ya dakika chache tukawa Delux, nikamlipa haki yake. Nilipoingia hotelini nilimuuliza mpokezi wa wageni kama alikuwepo mgeni wangu aitwaye George Chikaka toka Dar es Salaam.

"Yupo nambari 132 orofa ya kwanza".

"Asante".

Nilipanda ngazi kwa kukimbia. Nilitafuta chumba nambari 132 nikakiona. Nikanyata mpaka hapo nje, nikatega sikio. Nikasikia sauti ya Ole ikisema. "Sema umekuja na nani? Nakupa sekunde moja usipojibu utajua nitakufanya nini mbwa wee! Kafa Willy itakuwa wewe".

Nikashika bastola mbili mkononi nikaupiga teke mlango nikaingia ndani. Nikalenga bastola.

"Sijafa bado. Ole nipo na nitaendelea kuishi". Ndani kulikuwa na maiti tatu nikajua George walikuwa wamemshinda kwa taabu. Waliokuwa wamebaki ni Ole na mtu wake mmoja pamoja na George ambaye alikuwa amepigwa kiasi cha kufa wakati wowote.

"Tupa bastola yako chini". niliamrisha.

Walipokuwa wanataka kuweka chini bastola zao huyo mtu mmoja wa Ole akainua bastola yake kijanja lakini nikawahi kumuona na kumuwahi na kumpiga risasi akafa papo hapo.

"Ole, tayari umenisumbua kiasi cha kutosha na wewe pamoja na kundi lako lote mtalipa maisha ya watu wote mliowaua toka Jack Mbile mpaka George ambaye sasa amezirai na nimeamua kupambana na nyinyi ana kwa ana. Nani mkubwa wenu?"

"Sijui na wala usijidumbue kuniuliza. Mimi nilijua umekufa imekuwaje?"

"Unaleta utani?".

Niliweka bastola moja mfukoni nikamsogelea kusudi nimtwange, lakini kabla hata sijamfikia niliona macho yake kwa chati yanaangalia kwenye mlango na mara hiyo nikajua kuna kitu. Niliruka chini wakati tu risasi ilipopita hapo nilipokuwa nimesimama na wakati huo huo nikaachika risasi zikampata huyo mtu aliyetaka kuniua. Huku Ole alikuwa tayari akanirukia na kupiga teke bastola yangu, ikaanguka mbali lakini alikuwa amechelewa, mtu wake alikuwa amepatwa na risasi akaanguka na kufa. Ikawa kikiri mimi na Ole, tayari kwa mapambano.

Nilimrukia Ole kwa konde la shingoni akalikwepa na kunitandika konde la shingo nikayumba.

"Utanitambua leo", alisema na mimi sikujibu.

Alifululiza ngumi kama nne zikitoka kama umeme na zote zikanipata mpaka damu zikanitoka puani. Hiyo damu ikanisisimua.

Alitupa ngumi mbili tena mfululizo nikazikwepa na hapo hapo nikampiga konde la kifua akateteleka. Kabla hajajiweka sawa nikamtupia makonde mawili ya nguvu zangu zote kwenye kichwa akaanguka chini. Nikamrukia kumpiga teke la tumboni, akawahi kunishika na kunisukuma kwa nguvu nikaanguka chini.

Akanirukia hapo chini, yeye juu mimi chini. Akaanza kuninyuka. Kuona hivi nikatumia ujuzi wangu wa judo. Nikajipinda, miguu yangu ikamkaba shingoni

akapiga ukelele. Nikiwa tayari nimesimama na kabla yeye hajasimama vizuri nikampiga teke la mguu na nikauvunja, akalia.

"Aaa umenivunja mguu, niache inatosha".

"Haijatosha, nimekwambia lazima ulipe mateso ya rafiki zangu waliyoyapata".

Akajaribu kukimbia kwa mguu mmoja, nikaupiga ngwala huo mguu wa pili akaanguka chini kwa uchungu mwingi. Akalia.

"Basi imetosha".

Nilimwendea nikampiga teke la ubavu, nikaona amedhoofika kabisa. Nikaushika huo mguu uliovunjika, nikaanza kuunyonga.

"Aaa niache, niache! Niue tu kuliko kunitesa hivi".

"Nilifikiri wewe ni jasiri huwezi kusikia uchungu. Watu wote hao uliowaua uliwatia maumivu makali kabla hujawaua ulifikri wao si watu? Mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu. Utajua sasa".

Niliupinda tena mguu.

"Nani mtu wenu MWadui?"

Kwa uchungu akajibu.

"Watu wengi wa Mwadui wako kwenye orodha ya mshahara wa Pweke.

"Niambie jina la mtu mmoja mkubwa ambaye naye yuko kwenye hiyo orodha.

"Sikui".

Nikaupinda tena mguu.

"Aaa kweli sijui, Pweke ndiye anayewajua. Mimi ni mkubwa wa usalama wa kundi tu, sijui watu wanaoshughulika na wizi ila polisi wengi, afisa usalama na maafisa wengine wa juu nasikia pia wapo kwenye hiyo orodha".

"Pweke ana wenzake Shinyanga, Arusha, Mwanza, Musoma, Nairobu na Kampala, wote wako saba, nipe majiba yao.

Nikamuongezea maumivu. Hapo akaeleza.

"Busy yuko hapa Mwanza, Jonston Mwita yuko Musoma, Mashaka Athuman yuko Arusha, Shinyanga sijui mwingine ila ni huyo huyo Pweke, Nairobi Samweli

Gichuki, Kampala ni Tom Omandili na Dar es Salaam sijawahi kumuona lakini nasikia yupo."

"Nani mzee?"

"Kweli huyo simjui. Anayemjua katika kundi zima ni Pweke peke yake na hao wenzake hawamjua na wala hata hawajawahi kumuona.

Nikaamini maneno yake.

"Ulijuaje juu yangu na George?"

Niliambiwa na Pweke">

Kabla hajamaliza mlango ulisukumwa mimi nikaruka kando. Huyo jamaa aliyesukuma mlango akaachia risasi, zikamwingia Ole na kumuua. Mimi nikaachia risasi na kumuua vile vile. Nilipomwangalia George nikaona bado hajakata roho, nikarudisha mlango nikatelemka chini. Kufika mapokezi kijana wa mapokezi aliponiona nakuja akaanza kukimbia. Sikuwa na muda wa kuanza kumfuata ingawa ilionyesha kuwa hii Delux ilikuwa na uhusiano na haya majambazi. Nilipata teksi hapo nje ya Delux.

"Posta haraka sana".

"Shilingi kumi".

"Wewe twende, pesa siyo shida".

Aliondoa gari kwa kasi sana.

"Mswahili bwana anaweza kuingia ndani ya gari kiofisa bila kuuliza nauli, ukimfikisha aendako na ukimwambia nauli anaanza kubishana tena", alieleza dereva wa teksi.

"Inafuatana na mtu mwenyewe alivyo".

Wakati ninajibu tukawa tunafika posta. Nilitoa shilingi ishirini nikampa.

"Weka inayobaki".

Alhamndulilahi. Mungu akusaidie", dereva alishukuru.

Nilikimbia moja kwa moja mpaka kwenye simu, nikaweka senti hamsini.

"Sekou Toure Hospitali! Nikusaidie nini?" Opereta alijibu.

"Nipe daktari Makuyu".

"Subiri".

Daktari Makuyu alikuwa na mahusiano makubwa sana na idara yetu na aliletwa Mwanza kama daktari wa kawaida, lakini kiini hasa aliletwa kusaidia watu wa idara yetu, iwapo kuna matatizo na kuweza kutunza siri".

"Daktari Makuyu hapa".

"Gamba".

"Lo! Habari zako nimezisikia".

"Sawa, sasa fanya mbinu. George ana hali mbaya sana Delux Hoteli chumba nambari 132. Hali yake ni mbaya sana fanya haraka.

"Vema".

Akakata simu.

*****

Wengi tulimpenda sana Makuyu kwa namna alivyokuwa anafanya kazi. Kazi kwake ilikuwa kazi, si mchezo.

Nikapiga tena simu.

"Polisi Stesheni hapa", niliitikiwa.

"Nipe SSP Mwinyimkuu".

Subiri.

Nilingoja kidogo. baadaye sauti ikasikika.

"Mwinyimkuu".

"Ndani ya Mwanza Hoteli chumba nambari 230 kuna maiti na chumba nambari 132 Delux Hoteli kuna maiti vile vile. La kufanya utajua wewe mwenyewe. Pili mna mzigo humo uchukue ukae nao. Nitakupigia tena".

"Wewe nani?"

"Frend".

Nikaweka simu kabla hajajibu.

Nikazungusha nambari zingine za simu.

"Mahfudh yupo?"

Ndiyo".

"Nipe niseme naye"

Subiri.

Pakawa kimya kwa muda.

"Mahfudh hapa".

"Gamba".

"Lini uko huku?"

"Siku mbili hivi. Nipe Dar es Salaam upesi iwezekanavyo".

"Subiri".

"Mahfudh naye alikuwa amewekwa maalumu hapa Mwanza kwa nyakati kama hizi.

"Halo zungumza nao," Opereta aliniarifu.

"Maselina hujambo?".

"Nini wewe. Njoo upesi sisi huku tumekuota".

"Nipe Chifu".

"Subiri".

Kisha nikasikia sauti ya Chifu.

"Lete ripoti Gamba?"

"Watu wafuatao wawekwe chini ya ulinzi kwa usalama wa uchumi wa nchi hii. Jonston Mwita wa Musoma, Mashaka Athumani wa Arusha, Samweli Gichuki wa Nairobi na Tom Omandile wa Kampala. Watu hawa watafutwe wawekwe chini ya ulinzi mpaka baadaye. George yuko mahututi sijui kama atapona. Mtume Patrick sasa hivi kwa ndege mpaka Shinyanga halafu saa mbili jioni tuonane Maganzo".

Nilimweleza na mengine yote kwa muhtasari.

"Oke, nitamweleza Kamishna Mkuu wa Polisi ashughulikie habari hii. Nitaomba ndege ya serikali Patrick atakuwa Maganzo saa mbili".

"Sawa, atanikuta Maswa Bar".

"Oke, kwaheri"

Akakata simu.

Nilipomaliza kupiga simu nilijisikia mchovu na njaa iliniuma sana. Saa ilionyesha ni saa kumi na moja. Nilikuwa sina muda mrefu maana ilinibidi kwenda Maganzo nikamtafute Pweke ambaye ndiye aliyekuwa kiini cha kiunganisho cha wizi na ujambazi wote uliohusika na wizi wa almasi kutoka mwadui na kuuzwa kwa magendo Afrika Mashariki nzima. Niliingia kwenye mkahawa mmoja, nikanunua chakula cha kukaangwa na nikaomba wanifungie. Nilitafuta teksi ya kwenda Maganzo kwa haraka iwezekanavyo.

"Mbona shati lako lina damu kidogo nyuma umejiumiza?" Dereva wa teksi aliniuliza.

"Nashugulika na biashara ya nyama na huko nakwenda sehemu za Shinyanga kutafuta ng'ombe."

"Kazi ya fedha nyingi hiyo, nasikia."

"Wapi bwana, tunajaribu hivi hivi, tutafanya nini?"

Tukaendelea kimya. Baadae nikafungua kimfuko changu. Nikaanza kula chakula changu. baada ya hapo nikasinzia kwani nilikuwa nimechoka sana. Hatimaye dereva akanitikisa, nikaamuka.

"Halo, halo tumefika. Nilikwambia hii ni ndege, angalia sasa"

Na kweli huyu kijana alikuwa ameendesha kwa kasi sana maana ilikuwa saa kumi na mbili na nusu.

"Nipeleke Maswa bar".

"Hiyo bar ina vipande kweli kweli vya watoto, ukicheza nao si ajabu pesa yako ya kununua ng'ombe ikaisha kabla ya kwenda mnadani kesho asubuhi."

"Niko macho"

Baada ya kufika Maswa Bar nilimlipa dereva haki yake.

"Asanter sana. Sasa mimi narudi zangu Mwanza. Ukirudi nitafute tupige maji kidogo. Mimi kituo changu ni pale sokoni."

"Bila ya shaka"

Niliingia ndani ya bar. Nikatafuta meza moja nikakaa.

"Salama wewe bwana?"

Niligeuka nikaona ni yule yule mwanamke aliyekuwa amenipatia chumba siku ya nyuma yake.

"Salama Hujambo? Kwanza nipe ndovu baridi sana"

"Huu ubaridi unatosha?"

"Oooo sana tena."

"Mbona Hukuonekana tena?"

"Bwana we nilipata matatizo fuLani fuLani"

Kitu kilichonishangaza ni kwamba, bar ilikuwa imejaa watu kama kawaida, kama kwamba hakuna kitu kigeni kilichotokea ndani ya bar hii. Hii inanihakikishia kwamba hakuna habari yoyote iliyotokeza nje.

"Na leo unataka chumba?" niliulizwa na mpokea wageni.

"Ndiyo"

"Leo nafasi si kama za jana na juzi"

"Chumba cha mtu mmoja naweza kupata?"

"Ndiyo, bila ya wasiwasi, shilingi thelathini, nipe halafu nitakutafutia chumba chenye kitanda safi kabisa".

"Nitashukuru sana"

Nilitoa noti mbili za shilingi ishirini.

"Zitakazobaki kunywa soda"

"Asante sana" alijibu huku akiondoka kwenda kaunta.

SURA YA SITA

Nilikunywa bia yangu kwa utulivu kabisa. Nikafikilia mambo chungu nzima. Nilikata shauri nisifanye kitu chochote mpaka Patrick atakapofika maana hali ilivyokuwa sasa ilikuwa mbaya sana na kuikabili peke yangu ingeweza kuleta balaa. Hata hivyo nilihisi kwamba mpaka sasa nilikuwa nimefanikiwa kiasi kikubwa sana, maana nilikuwa nimeshapata fununu za ujambazi huu, kiasi kilichobaki ni kutafuta shina. Matawi ya ujambazi nilikuwa nimeanza kuyakata. Yalikuwa ni matawi machache makubwa makubwa pamoja na shina ndivyo vilivyokuwa vimebaki. Nilijua kuwa kuling'oa shina haikuwa kazi rahisi, kwa hivi ilibidi nipange mambo vizuri na ndiyo sababu ilinibidi nimngoje Patrick maana wawili ni wawili.

"Njoo uone chumba chako aliniita huyo mama.

"Ngoja nimalize bia yangu."

"Twende nayo mimi nitakuchukulia"

"Haya twende"

Alinichukulia bia tukaelekea chumbani. Chumba kilikuwa kifinyu lakini kusema kweli kilikuwa na kitanda kizuri na kikubwa. Nilikagua dari nikaliona imara maana nilikataa mambo ya siku iliyopita yasinitokee tena.

"Chumba hiki unakionaje?"

"Safi sana"

"Kitanda je?"

"Safi kabisa"

"Lakini kinafaa kuwa na mwenzi wa kuongea naye."

"Bila shaka sina haja ya kwenda mbali ili mradi wewe upo. unasemaje?"

"Aka babu, Mimi bwana wangu leo anakuja kunichukua. jana ndipo ungenipata maana alikuwa Mwanza lakini leo karudi".

"Kwani huwezi kumkacha?"

"Loo, nimkache shauri yako! Waswahii husema usiache mbachao kwa mswala upitao. Yule bwana ananifaa. Ananilipia kodi ya nyumba, ananunua chakula na analipa maziwa ya mtoto. Leo nikimkacha kwa kukufuata wewe, utanipa tuseme shilingi ishirini, hata mia, halafu kesho asubuhi huyo unakwenda zako. Nani atanilipia kodi ya nyumba, maana bwana wangu atakuwa naye kisha nikacha"

"Sawa bibi umeshinda. Nitapata wasio na wao"

"Bila ya shaka utapata, kijana nadhifu kama wewe utakosaje?

Ulipoingia tu kwenye baa kila mwanmamke mle ndani alikuwa anakukodolea macho. Unafikiri asingekuwa huyu mlipa kodi ningekuachia? Ng'oo".

"Naenda kukoga".

"Haya, utanikuta ndani ya baa".

Ilikuwa yapata saa moja nilipomaliza kukoga. Shati langu nililifua hapo penye damu, halafu nikapakausha kwa kupanyonga na taulo nikalivaa. Sasa nilikuwa najisikia vizuri zaidi baada ya kukoga. Nikakata shauri kwenda baa nikamsubiri Patrick.

Nilipoingia ndani ya baa moyo wangu ulishituka kidogo. Nilipotazama huku na huku nilimuona yule msichana ambaye nilikuwa nimemuona Mwanza Hoteli mchana. Alikuwa amekaa peke yake akinywa. Alinitazama na macho yetu yakapambana akainamisha kichwa. Alikuwa msichana mzuri nikakata shauri kumsogelea.

"Habari zako dada?"

"Nzuri" alijibu kwa sauti tamu.

"Nilikuona leo mchana Mwanza Hoteli kama sikukosea".

Alishangaa na kunyamaza. Bia yake ilikuwa nusu kwa hiyo nikamwita mwanamke wa baa alete chupa mbili moja yangu na moja ya dada.

"Mimi hapana, nitaondoka sasa hivi", alijibu huku akiniangalia kwa chati.

Sikutaka kujirahisi kwa kusisitiza.

"Oke lete moja. Umefika hapa saa ngapi?"

"Sasa hivi".

"Na nini?"

"Ninaendesha gari".

Nilipomwangalia vizuri ndipo nikakumbuka kwamba nilimuona Mwanza siku ya ajali ya boti itokayo Ukerewe, ambamo alikuwemo Makungu Majula. Dada huyu ni peke yake aliyepona".

"Unaelekea wapi?"

"Nimekuja kumuona rafiki yangu mmoja hapa".

"Kwani unakaa wapi?"

"Mwanza".

"Mimi naitwa Mark, wewe unaitwa nani?"

"Tausi".

"Samahani, sijui ndiye wewe uliyepona kwenye ile ajali ya boti iliyokuwa ikitoka Ukerewe kwenda Mwanza, maana sura iliyokuwa kwenye gazeti inafanana sana na yako?"

Alitabasamu.

"Ni mimi. Magazeti haya yanaleta shida, kila mtu akiniona anasema msichana huyu ana bahati, watu wote walikufa kapona yeye tu".

"Hawajui Mungu hapendi kuua viumbe wazuri kama wewe. Ungekufa nani angekuwa anazungumza na mimi sasa?"

"Samahani naenda Farmera Bar, ndipo rafiki yangu anakonisubiri saa moja na nusu.

Nilifikiri kidogo kama ningemwacha aende au sivyo.

"Naweza kwenda nawe? Ningependa kufika huko lakini nitarudi hapa saa mbili.

NIlilipa pombe tukaongozana nje.

"Gari hilo hapo."

Alifungua mlango wa dereva halafu akanifungulia mlango wa mbele wa abiria. Nikaingia ndani kwa chati nikaangalia nyuma hamkuwa na mtu wala kitu chochote. Akatia gari moto tukaondoka na kuingia barabara kuu. Kisha nikasikia sauti kwa nyuma.

"Kaa hivyo hivyo usijisogeze hata inchi moja, ukijisogeza tu umekufa. Tausi moja kwa moja mpaka ulikoambiwa. Mara hii atarukoma ng'ombe huyu".

Kijasho kilinitoka sikuwa na la kufanya. Nilipotaka kukaa vizuri tu, nikatwangwa na kitu fahamu zikaniruka. Nilisikia kwa mbali watu wakizungumza. Nikajaribu kuinua kichwa lakini sikuweza. Kilikuwa kizito sana.

"Mmwagie maji apate fahamu. Nataka kuzungumza naye".

Nilimwagiwa maji ya baridi sana. Haya yalinipa nguvu nikainua kichwa na kufunua macho. Mikono na miguu yangu ilikuwa imefungwa kwenye kitu imara sana. Ndani ya hiki chumba mlikuwa na watu watano. Nilimtambua Pweke mara moja maana nilikuwa nimekwisha kumuona Songwa Club. Tausi alikuwepo pamoja na watu wengine watatu, ambao wote walikuwa wameshika bastola zao tayari tayari. Chumba nilichokuwemo kilikuwa kifinyu sana. Kilikuwa na mlango mdogo wa kuweza kuingia mtu mmoja mmoja. Kilikuwa na madirisha mawili madogo juu kabisa ya dari na hewa ilikuwa ya baridi na safi kwa vile chumba kilikuwa kinatumia mashine ya kufanya hewa iwe baridi.

"Willy Gamba au Mark Buhulula hujambo?" Pweke alisalimu kwa kebehi.

"Asante sana Pweke ama nani sijui".

"Usitake kujua maana hata ukijua ni kazi bure, mwisho wako ni leo".

"Mwisho wangu unaweza kuwa leo, lakini serikali yangu haina mwisho. Nitakufa leo, kesho atatokea tena mtu mwingine kuliko mimi na ataendelea na pale nilipoishia. Umeua watu wengi mbona bado tunaendelea tukianzia pale walipoishia walipoishia.

"Sawa, lakini kicho chako kitakuwa tisho kubwa kwa serikali. Itabidi itulie kidogo kabla haijachukua hatua nyingine na wakati huo tutafanya jitihada ya kunyakua kiasi cha kutosha na kutulia".

"Usijidanganye. Mikifa mimi utakuwa ndiyo umeweka kiberiti kwenye petroli".

"Umeua watu wangu wengi sana, kwa hivi itabidi upate mateso ya peke yake. Lazima upate uchungu, ujutie nafsi yako - kwanini umekuwa unatufuatafuata. Hii shughuli toka nianze sijatiwa msukosuko kama huu, kwa hivi hasira yangu imepanda mpaka imefurika na lazima ulipe watu wangu wote uliowaua hasa Ole.

"Na wewe siku ya kukupata utalipa mauaji ya wote uliowaua toka Jack Mbwile mpaka utakayekuwa umemuua wakati huo".

"Unatania, mambo yangu yameshatengamaa. Baada ya usiku huu wa leo naweza kuondoka na kuishi mahali pengine popote ulimwenguni bila ya taabu. Mali niliyonayo hata wajukuu zangu wanaweza kula bila ya kufanya kazi. Usiku huu wakati wewe umeshaaga dunia sisi tutakuwa tunagawana almasi yenye thamani ambayo serikali itapata pigo kubwa sana, pigo ambalo haitasau, pigo ambalo litafanya hata Kampuni ya Almasi ifungwe. Ni wewe tu ambaye kidogo utuharibie.

"Saa zimekaribia, fanya twende. Nafikiri wengine watakuwa wameisha wasili", Tausi alisema.

"Na wewe bibi umejiunga ndani ya kundi hili?" niliuliza.

"Hujui ni miaka ya wanawake?"

"Miaka ya wanawake katika kuendeleza nchi au kubomoa?"

"Wako wengine wanajenga wengine wanabomoa. Mimi ninajenga peke yangu.

"Lazima ujue kuwa utalipa kifo cha rafiki yangu Makungu Majula pamoja na wananchi wote waliokuwa ndani ya ile boti. ni aibu kuona msichana mzuri kama wewe unashiriki kikamilifu katika uovu na watu washenzi na vichaa kama huyu Pweke na wenzake. Huyu si mtu tena ni mnyama.

"Nyamaza ng'ombe".

Pweke aliniwasha kofi la usoni na Tausi akanirukia na kunitia makucha uso mzima na damu ikaanza kububujika.

"Ukome kama ulivyokopa kunyonya titi la mama yako", Tausi alitukana.

"Basi na mimi niachie nnimuonyeshe uchungu wa rafiki zangu aliowaua kabla hatujamuua", mmoja wa hao vikaragosi wa Pweke aliomba.

"Haya chukueni nafasi zenu na kila mtu mmoja amalize uchungu wake. Msimuue kabisa niachieni mimi ndiye nitammalizia".

Walijiweka sawa na kuanza kunitwanga. Damu ilikuwa inabubujika machoni kutokana na makucha aliyonitia Tausi. Sikuwa naweza hata kuona. Nilikuwa nimefungwa kistadi kiasi cha kwamba nisingeweza kufanya chochote. Nilipigwa makonde ya mashavuni, kifua na tumboni, mwingine aliruka na kunitwanga teke la mbavuni. Hasira zilinipanda kiasi ambacho sijawahi. Niliwachukia kiasi cha ajabu.

"Mtalipa, hakika mtalipa na mtalipa ghali sana", nilipiga kelele kwa uchungu mwingi.

"Ha ha ha Willy Gamba mpelelezi mashuhuri analia kama mwanamke. Ha ha ha ha! Niachieni sasa mimi nimmalize", Pweke alisema kwa dharau.

"Lakini mzee alisema anataka kumuona kabla hatujammaliza kabisa", Tausi alisema.

"Atafika hapa si muda mrefu lakini hata hivyo alimtaka akiwa amekufa au yu hai kwa hiyo mimi ninakata shauri nipeleke maiti yake."

"Ngoja kwanza Pweke na mimi nimfaidi kabla hatujammaliza", Taus alisema.

Tausi alinirukia na kunitia makucha kifuani na tumboni na kuraruaraua shati langu nililokuwa nimevaa. Uchungu niliopata ni Mungu na mimi mwenyewe ndio tunaojua. Nguvu ziliniishia, nilikuwa siwezi hata kusema na nilijua mwisho wangu umefika.

Damu zilinitoka kila mahali. Nikaanza kupoteza fahamu. Ghafla taa zikazimika, maana nilikuwa naweza kuona wekundu lakini ghafla kukawa giza. Mashine ya kufanya hewa baridi ikanyamaza. Kufumba na kufumbua nikatumia nguvu zangu zote zilizobaki. nikajitupa upande na kuanguka chini pamoja na kiti nilichokuwa nimefungiwa.

"Tumeingiliwa. Muue upesi, ng'ombe nyinyi. Hakikisheni mnamuua sitaki kusikia yu hai", nilimsikia Pweke anapiga kelele kwa woga. Nilisikia kwa kutoka juu dirishani risasi zinamiminika halafu nikapoteza fahamu.

Nilipozinduka nikajikuta kwenye chumba kidogo, nikiwa nimelazwa kitandani na huku nimefungwa bandeji kila mahali nilipokuwa nimeumia na nilipoinua macho karibu yangu alikuwa ameketi msichana mrembo sana huku akitabasamu nikashangaa.

"Unajisikiaje sasa?" Aliniuliza.

Nikatabasamu.

"Mbele ya mtoto mzuri kama wewe nitashindwaje kujisikia vizuri".

"Watu wa hali yenu ni watu wa ajabu sana".

"Kwanini?".

"Hata hushangai umekujaje hapa?".

"Ili mradi nimetibiwa na msichana mrembo kama wewe, na unaniganga na hakuna watu wenye sura zilizokunjana wakiwa wameshikiria bastola, najua niko kwenye mikono mizuri".

"Ni kweli".

Nilijaribu kuinuka.

"Daktari amesema upumzike kwa muda mpaka upate nguvu".

"Tayari nina nguvu, sasa ni saa ngapi?"

"Saa saba unusu usiku".

Nikatambua kuwa nilikuwa nimezirai kwa muda wa masaa matano hivi na nikataka kujua nini kilikuwa kimenitokea muda wote huo ili niweze kujua nini cha kufanya maana hata hapa nilipokuwa sikujua ni wapi na huyu msichana sikujua ni nani.

"Wewe ni nani na hapa ni wapi?"

"Mimi naitwa Amanda Mwakasege, na hapa ni nyumbani kwa rafiki yangu, Songwe Madukani.

"Nani alinileta hapa?"

"Mimi na Patrick".

Moyo wangu ulishtuka kwa jina hilo.

"Yuko wapi?"

"Amerudi Maganzo na atarudi wakati wowote".

"Kwa hiyo nyinyi ndiyo mlioniokoa kutoka mikononi mwa Pweke?"

Bila shaka".

Hii ilinishangaza sana.

"Nafikiri uko tayari kunieleza juu yako mwenyewe na jinsi gani unahusika katika kesi hii, maana wewe hukuajiriwa pamoja na sisi. Vile vile jinsi gani mlijua nilipokuwa na vile mlivyoniokoa".

"Nitakueleza kwa ufupi ili uweze kujua mpaka sasa pilikapilika yako hii imefikia wapi".

"Asante, endelea".

"Mimi naitwa Amanda Mwakasege, kama nilivyokwisha kukueleza. Ni Mwandishi mahsusi wa Meneja wa Kampuni ya Mwadui. Utashangaa nimejiingizaje katika jambo hili au sivyo?".

"Nina mshangao mkubwa sana, maana ukiwa mwandisi halafu ujiingize kwenye jambo la hatari namna hii haieleweki."

"Kweli haieleweki. Mimi nilikuwa na mchumba wangu akiitwa Inspekta Joel Zonga, nafikiri uliwahi kumsikia?|

"Nilikuwa nimesikia habari zake ambazo zilitokana na kifo chake. Alipata ajali ya ndege iliyokuwa mali ya Kampuni Mwadui alipokuwa akisafiri kwenda Mwanza kikazi. Mpaka leo chanzo cha ajali hiyo hakikujulikana maana ndege ilipasuka vibaya mno. Polisi walikisia kuwa mlikuwa na bomu lililotegwa lakini hawakuweza kuendeleza upelelezi wao mbali".

"Ndivyo ilivyokuwa."

"Pole sana".

"Siku moja Joel alikuja nyumbani kwangu akiwa na mawazo mengi sana. Nilitengeneza chakula lakini hakuweza kula vizuri. nikajua alikuwa na kitu kilichokuwa kinamsumbua nilimdadisi sana mwishowe akanieleza. Alinieleza ya kwamba alikuwa hapendezewi na jinsi mambo yalivyokuwa yakienda hapo Mwadui na kwamba alikuwa ameamua kufanya uchunguzi madhubuti.

"Alinieleza kuwa alikuwa amefanya uchunguzi kiasi na kuona ya kwamba kulikuwa na mpango wa hali ya juu sana wa kuiba almasi toka Mwadui! Ila alisema kilichokuwa kinamkera ni kwamba angeweza kuwa hatarini.

"Alieleza ni nini kilichomfanya afikiri hivyo?"

"Alikuja kunieleza baadaye. Aliendelea na uchunguzi wake na hatukulizungumzia jambo hili tena. Baada ya miezi miwili hivi siku moja alikuja akiwa na hali isiyo yake ya kawaida. Nilipomuuliza alinieleza ya kwamba mambo aliyokuwa anafikiria ni kweli na sasa alikuwa hatarini.

Alinieleza kwamba alikuwa amekata shauri kunieleza jinsi mambo yalivyokuwa kusudi ikiwa jambo lolote likimpata siku moja anaweza akaja mtu mwenye kuweza kuendeleza upelelezi huu na habari hizi zingemsaidia sana. Nilimwambia asiseme hivyo, na siku hiyo alilia sana.

"Alieleza nini?"

Alinieleza kuwa maafisa wengi wa polisi wa chini wa hapo Mwadui walikuwa wamehongwa na kundi la majambazi ambalo lilikuwa linaendelea na kuendesha wizi wa hali ya juu wa almasi toka Mwadui na ndiyo sababu hali ya uchumi utokanao na machimbo hayo ya almasi ulizidi kwenda chini siku hata siku.

"Alisema kuwa hili kundi lilikuwa limepachika watu wake kila idara na kila sehemu zinazohusika na almasi. Na hawa watu ndio walikuwa wakitorosha almasi kidogo kidogo na kwa sababu polisi waliokuwa wanahusika wote wamehongwa na walikuwa wanawajua basi ilikuwa rahisi sana kwao kutorosha almasi.

"Alinieleza kuwa katika miezi hii miwili aliweza kukamata watu kama kumi ana kwa ana na almasi mkononi lakini alipoenda kupiga ripoti kwa maofisa wa juu waliweza kutaka hata kumgeuzia yeye kuwa ndiye mwizi. Hata akanieleza kuwa siku moja wamewahi kuficha almasi nyumbani kwake halafu kukafanywa uchunguzi zikutwe kwake lakini yeye alinong'onezwa kabla na rafiki yake mmoja na walipofika hawakukuta kitu.

"Kutokana na uchunguzi wake alikuwa amegundua kuwa kwa nje kulikuwa na mtu aitwaye Pweke, ndiye alikuwa mkubwa wa kundi na alikuwa mfanyabiashara wa hapo Maganzo. Kwa ndani mtu aliyekuwa akiongoza kundi Inspekta Mwandamizi Khamis Omari. Huyu Khamis ndiye aliyekuwa anapokea habari na ndiye aliyekuwa kiungo kati ya kundi la nje na la ndani. Vile vile kwa wafanyakazi wa idara zingine".

"Kwanini hakupeleka habari hizi kwa Mkuu wa Polisi wa Mwadui au Mkuu wa usalama?"

"Alisema alijaribu kupeleka kwa Mkuu wa Polisi, lakini alipuuzwa na kuelezwa kwamba alikuwa anaanzisha majungu jambo ambalo serikali haipendi hasa jeshini na kwa hivi angeweza kuchukuliwa hatua. Alipoona hivi akaonelea aendelee kufanya uchunguzi wake yeye mwenyewe sasa. Siku aliyokuwa amekuja kwangu na huzuni kunieleza mambo haya ndiyo siku aliyokuwa amekuja kwangu kunieleza kuwa amepata kitisho kutoka kwa mtu aliyekuwa akiitwa Elungata akisema asiingilie mipango yake la sivyo maisha yake yangekuwa mafupi sana".

Jina la Elungata mara moja nilikumbuka kwani marehamu Matayo Buluba alikuwa ameniletea barua kutoka kwa marehemu Jack Mbwile na hiyo barua ilikuwa na neno moja tu 'Elungata' Sasa nilianza kuona mwanga zaidi.

"Aliweza kuchunguza na kujua huyu Elungata alikuwa nani?".

"La hasha. Baada tena siku moja kwenye Mkahawa wa polisi hapo Mwadui alinieleza kuwa alikuwa amegundua tu ya kwamba Pweke siyo mkubwa kabisa wa kundi ila mkubwa alikuwa Elungata, lakini ajabu huyu Elungata hata hakuweza kupata fununu yake".

Wiki tatu zilizopita akaja siku moja kuniaga kuwa alikuwa anaenda Mwanza kuonana na Mkuu wa Polisi wa Mwanza ampe habari hizi kwa maana sisi tulikuwa tumekata shauri ya kuoana baada ya mwezi mmoja toka siku hiyo kwa hiyo asingekuwa na nafasi ya kuendelea na uchunguzi. Na siku hiyo alipoondoka ndiyo waliyomtega bomu katika ndege. Akafariki".

Alianza kulia. Nilimvuta na kuanza kumbembeleza.

"Basi, basi kifo ni mapenzi ya Mungu. Ni jambo la kusikitisha sana lakini kulizuia hatuwezi. Yeye alipangiwa na Mungu mwisho wake uwe huo. Ulikuwa mwisho wa fahari maana alikufa kwa sababu ya kupenda nchi yake na kwa kuitumikia vizuri. Maadui wa maendeleo yetu wamemuua. Kwa hilo linalotupasa mimi na wewe ni kuwafutilia mbali hawa maadui wa nchi yetu".

"Asante Willy lakini ni vigumu kusahau na vile vile ndiyo sababu nimejitoa mhanga wa kufa na kupona kusudi watu waliomuua mpenzi wangu Joel na wao watiwe nguvuni".

"Joel alikueleza haya yote kwa sababu alijua atakuwa hatarini na alifanya vizuri. Je umetimiza wajibu wako kwa mzigo aliyekuachia?".

"Nafikiri leo hii na dakika hii nimetimiza wajibu. Hata hivyo baada ya mazishi na matanga sikukaa bure. Uchungu niliokuwa nao ulifanya nami nianze uchunguzi wangu. Inspekta Mwandamizi Khasimu Omari ambaye ndiye bila shaka aliyepanga kuuawa kwa mpenzi wangu Joel alikuwa akitaka mapenzi nami siku nyingi. Niliporudi tu kazini baada ya matanga alianza kunifuatafuata".

..."Alinieleza kuwa ili niweze kusau mapema kifo cha ghafla cha mpenzi wangu ilinibidi nipate mtu wa kunifariji kwa sababu nilikuwa najua habari zake, wazo lilinijia kuwa ningeweza kupata habari za kunisaidia kuchunguza kifo cha mpenzi wangu joel".

"Kwa hiyo ukamkubali!"

"Nilimkubalia kwenye mdomo tu si rohoni".

"Sawa".

"Siku moja nilianza kwa kumsifu juu ya vile alivyo tajiri kuliko polisi wengine, jinsi alivyokuwa na akili kuliko polisi wengine na kadhalika. Nilimweleza kuwa ningejua kwamba yeye ana pesa hivyo hata nisingejisumbua kupoteza muda wangu na Joel. Nikamweleza kuwa ni bahati nzuri upande mwingine kwamba Joel amekufa. Hii ilimfurahisha sana akaanza kujitapa akanieleza kuwa yeye alikuwa tajiri sana na utajiri wake usingeweza kupungua kwani alikuwa ameishashika Mwadui nzima mkononi mwake."

"Siku hiyo nilimfanyia mapenzi ya kila aina mpaka akanieleza juu ya siri zake. Akanieleza baada ya muda si mrefu angeacha kazi na kunioa halafu tungeenda kuishi nchi za nje. Aliniambia ana almasi chungu nzima. Nikamkebehi ya kwamba mbona nasikia kwamba Pweke ana hela kuliko yeye. Akacheka na kusema bila ya yeye Pweke si kitu".

"Hakugutuka kuwa unamfahamuje Pweke?".

"Asingeweza, maana Maganzo nzima wanamfahamu Pweke. Ana pesa chungu mbovu. Wakati wote huu nikawa natafuta njia ya kujua mengi lakini sikuweza kuwa na bahati. Waswahili husema mvumilivu hula mbivu, kwa hiyo mimi nikaendelea kumganda nikisubiri bahati yangu huku nikimlaghai kwa mapenzi kwa kweli ya Mungu mengi jana ndiyo siku yenyewe.

"Jana alikuja nyumbani kwangu huku jasho likimtoka. Nikatengeneza chakula kama kawaida, lakini hakuweza kula na alionekana na wazo linalomsumbua au tuseme mawazo yalikuwa mengi sana. Nilimuuliza nini kilikuwa kinamsumbua. Hakutaka kunieleza. Nikazidi kumbembeleza. Nikambusu, nikamweleza kuwa matatizo yake ni yangu na mimi kwa vile nilikuwa nimekata shauri la kuolewa sikuona kwa nini anifiche jambo lolote hata kama ni kuua mtu.

"Mwisho akanieleza kuwa mpelelezi mmoja maarufu wa serikali kwa jina la Willy Gamba alikuwa ameanza kuleta matatizo. Nikamwambia mtu mmoja tu si kitu, hatamudu kufanya lolote, kwa hiyo asijali hata kidogo. Basi akafurahi akanishika akanibusu.

"Akanieleza kwamba ameonelea lazima achukue livu kesho yake maana tungeweza kuondoka ghafla kwa muda. Nilimwambia kwamba isingekuwa taabu.

SURA YA SABA

Moyoni nikajua nafsi yangu imefika ya kumtafuta huyu Willy Gamba ili nimweleze yote niyajuayo ili kwamba nitakuwa nimemlipizia kisasi mpenzi wangu Joel."

"Ama kweli umekuwa kiumbe wa ajabu! Umeweza kufanya yote haya kwa ajili ya mpenzi wako Joel basi".

"Nakwambia, watu hawajui. mwanamke akipenda kitu huvumilia sana usituone hivi!"

"Kweli nami nimeona kitu kiitwacho mapenzi ya kweli maana mtu kafa na bado anapendwa tu".

"Basi leo asubuhi nikaenda ofisini. Nikachukua livu, nikampigia simu sikumpata kwa simu ofisini wala nyumbani. Nikakata shauri kwenda nyumbani kwake sikumkuta lakini mimi nina ufunguo mwingine wa nyumba yake nikaingia ndani, nikaenda chumba cha kulala nikachukua bia, nikajilaza kitandani nikinywa huku mawazo yakinitembeatembea.

"Mnamo saa sita hivi nikasikia watu wanacheka ukumbini nikasikia mwingine akisema Willy kafa kifo cha kijinga sana cha kugongwa na gari moshi. Khasimu akajibu, ndiyo, sawa hiyo, hakuna hata cha kuuliza. Basi roho yangu ikafa kabisa niliposikia hivyo. Nikajua matumaini yangu yamekwisha".

"Naona nina maisha marefu," nilisema kwa furaha.

"kweli una maisha marefu. Khasimu aliponikuta chumbani akaja akanibusu. Nikamuonyesha karatasi zangu za livu. Akaniambia kwamba sasa hamna wasiwasi, tungepanga mambo yetu taratibu. Wakati bado tumekaa, simu ikalia. Alienda kuzungumza na nikasikia akisema, George, basi wamalizie mbali mbali na yeye halafu hana wasiwasi Ole yuko Mwanza, atamaliza tatizo hilo halafu akarudi".

"Na katika watu wanaovumilia wewe nambari moja!" Nilimpongeza, "Wanawake kwa kawaida wangekuwa wameisha ropoka".

"Kila nikimfikiria Joel, roho yangu inakuwa jasiri sana. Mnamo saa kumi na moja na nusu hivi simu ikalia. Khassimu alikuwa amelala akaamka na kwenda kuijibu. Nikasikia akisema kwa hasira, nini? Willy yuko hai? Willy au jina lake? Nani,

Ole? Ole kafa! lo, mambo yameharibika. Washenzi hao Pweke hakikisha Willy akiingia Maganzo Bar, ndiyo hoteli yake, lazima auawe mara moja. Nani kakupa habari? Basi lazima atafikia Maswa Bar, ndiyo hoteli yake kama atakuwa kaondoka kule saa kumi na moja, saa moja hivi atakuwa Maganzo. Mtume Tausi saa moja pamoja na kundi, yeye ni mbovu sana kwa wanawake. Lazima akimuona tu Tausi hawezi kumwachia. Mpeleke kwenye banda mkiweza kumkamata, mwuweni huko huko. Mimi nitazungumza na mzee najua atakasilika sana. Tuonane kwenye chumba chetu Bantu. Wengine wote watafika saa nne usiku kwaherini!"

"Kisha akaja akaniambia, mpenzi fungasha nguo zako chache na zangu mimi nitarudi kwenye saa tano au sita hivi nina shughuli.

"Nikamwambia, hamna taabu. Alipoondoka tu na mimi nikaanza kutafuta njia gani ya kuwahi kufika Maganzo kabla ya saa moja niweze kukupa tahadhari. Nilitafuta gari mpaka kwenye saa moja ndipo nilipopata. Kufika Maganzo na kuingia Maswa Bar saa moja na nusu, na nilipoangaza angaza nikaona hakuna dalili ya mtu kama wewe. Nikajua tayari wamekuwahi. Nikajua wamekupeleka kwenye banda. Na banda mimi nililijua, nilishapelekwa na Khasimu, lakini kukufuata peke yangu ilikuwa haiwezekani. Nikatoka nje ya baa, nikaanza kulia. Bado machozi yananitoka nikaona taksi inasimama na anatoka mtu na mfuko. Moyo ukanieleza ndiye wewe, nikamkimbilia huyu mtu. Bila ya hata kuogopa nikamuuliza kama yeye ni Willy Gamba? Akashituka na kuniuliza, 'kwanini?' Nikamwambia wanakutafuta watakuua. Wanajua utakuja hapa bila ya shaka.

Alinivuta kando, kisha akanieleza kuwa yeye anaitwa Patrick na ni rafiki yake na Willy Gamba. amekuja kukutana na Willy hapo. Ndipo nikamweleza mipango yao yote. Akafungua mfuko wake, akatoa bastola mbili. Akazijaza risasi akaniambia nimuonyeshe hilo 'banda' lilipo. Basi nikampeleka mpaka kwenye banda. Hii nyumba inayoitwa 'banda' imejengwa mbali kidogo na nyumba zingine. Khasimu alisema hutumika kama kuna sherehe fulani ya vinywaji. Basi nikamleta na kumuonyesha nyumba akanipa mfuko na tukaanza kuinyemelea nyumba akiwa na bastola mbili tayari.

"Upande wa mlango wa kuingilia, tukamuona mtu na bunduki, Patrick akamnyemelea akampiga konde la shingoni, akazirai bila ya kutoa sauti. Mwingine alikuwa akiangaza upande mwingine, Patrick akamwahi na risasi lakini bunduki haikupiga kelele. Ndipo katika kusikiliza akasikia sauti inatokea kwenye chumba walichokuwa wanakutesa. Alipoangaza akaona dirisha juu kabisa. Akapanda juu

kama nyani. Alipofika juu alipiga waya wa umeme na wakati huo huo alikuwa ameishawaona walivyokaa na wewe uliko kwa hiyo ilikuwa rahisi kuwawahi hao wenye silaha. Anasema usingejitupa na kiti wangeweza kukupata na risasi. Wale watatu wenye bastola wote amewaua. Pweke na Tausi wamekimbia. Basi Patrick akaniita, akakufungua, tukakubeba na kukuweka kwenye gari la Tausi. Patric akafungua boneti akaliwashia huko hadi tukafika hapa.

"Hiki ni chumba cha rafiki yangu, anafanya kazi stesheni ya reli hapa Songwa lakini yuko likizo. Tulienda kumtafuta daktari akaja akakutibu na akasema hukuvunjika chochote ila tu umepoteza damu nyingi. Akaomba upumzike mpaka kesho asubuhi utapata nafuu. Hivi ndivyo ambavyo tumeweza kuonana. Ni hadithi ndefu au sivyo?"

"lO, ama kweli ni ajabu na kweli. Sina budi kukushukuru sana"

"La hasha! usinishukuru. Nifanyalo ni wajibu wangu ili kulipiza kisasi cha Mpenzi wangu Joel!"

"Hakukueleza Patric yuko wapi?"

"Amewafuata Bantu ambako walisema wataonana"

"Ameenda pekee yake? Watamuua ni watu wabaya sana"

"Hapana, ameenda na mdogo wa yule daktari maana wao pia wanakisasi na Pweke maana alikataa kufanya mapenzi nao na huyu kijana ni Polisi wa relwe"

"Bado haitoshi lazima niwafuate"

"Una silaha? Silaha huna tena bado una maumivu. Wily usiende Patric na huyo kijana Mungu atawasaidia na watamudu"

"Silaha nitapata usijali lazima niwafuate.

Nikasikia sauti nje ya mlango wa chumba.

"Huna haja ya kuwafuata"

Jasho likatutoka wote.

Mlango ulifunguliwa wakati mimi nikiwa tayari kwa lolote litakalotokea na kwa mshangao wangu Patrick aliingia ndani. Niliruka hapo nilipokuwa.

"Patrick!".

"Willy".

Tukakumbatiana.

"Na nyinyi nanyi! Mnapendana hivyo?" Amanda alisema.

"Usijali," nilimjibu.

"Yule mdogo wa daktari yuko wapi?" Amanda aliuliza kwa woga.

"Yupo atakuja," Patrick alijibu.

"Patrick nipe habari kwa ufupi maana nimekuwa nje ya hii shughuli kwa masaa kwa hiyo niko nyuma sana na habari."

"Nafikiri Amanda kishakueleza jinsi tulivyokupata."

"Ndiyo, kanieleza."

"Huko Dar es Salaam nilipata habari kama saa kumi na moja unusu hivi Chifu alinieleza kwa ufupi juu ya habari zote na maendeleo ya shughuli hii. Mambo mengine yote alimweleza Kamishna Mkuu wa Polisi ashughulikie kama vile kuwatia nguvuni hao majambazi uliokuwa unawakisia. Mimi aliniambia niwe kiwanja cha ndege saa kumi na mbili kamili tayari kwa kuondoka.

"Wakati nikiwa kiwanja cha ndege nikapata habari toka kwa Chifu kuwa Kamishna Mkuu wa Polisi ndugu Oswald Mengi kapata safari ya ghafla. Maana baada ya kuongea na Chifu alipata habari kuwa mkewe aliyekuwa anasafiri toka Arusha alikuwa amepata ajali kati ya Arusha na Moshi na inasemekana kuwa huenda amekufa kwa jinsi hii ameruhusiwa kwenda kumuona mkewe kwa hiyo sasa mambo yote yako mikononi mwa Chifu na Mkurugenzi wa Upelelezi, Mkuu wa Polisi ameitwa arudi haraka maana jambo hili limefikia hatua ya juu haliwezi kushughulikiwa na maafisa wa chini wa polisi.

"Baada ya kupata habari hizi nilipanda ndege ya jeshi na mnamo saa moja unusu nilikuwa Maganzo na ndipo nikaonana na Amanda. Mambo mengine yote nafikiri kesha kueleza."

"Nipe habari za Bantu Bar".

"Baada ya kukuleta hapa nilionelea niwafuate kwa kufuatana na habari nilizopewa na Amanda. Huyo mdogo wake daktari akasema twende naye nami nikaona bora. Tulipofika hapo tulipeleleza uwezekano wa kuwepo huo mkutano lakini hakukuwa na dalili. Tulingoja sana lakini hatukuonana dalili yoyote. Tukajua kwamba lazima kulikuwa na mabadiliko ya mipango."

"Mlingoja mpaka saa ngapi?".

"Mpaka saa tano unusu hivi. Mimi nilionelea nirudi nikamuacha Wilfed Mbogo ambaye ndiye huyo mdogo wake daktari aendelee na uchunguzi na apatapo habari yoyote aje kutueleza kabla sijaja nikaonelea nimpigie simu Chifu, nimweleze tumefikia wapi na mambo yalivyo. Nilipiga nyumbani kwake nikapata habari kuwa amerudi ofisini. Hii ilinishangaza. Nikampigia ofisini.

"Nilipompata nikamweleza mambo yalivyo mpaka dakika hii. Kisha nikamuuliza kwanini alikuwa ofisini mpaka dakika hiyo. Akanieleza kuwa alikuwa amepata habari zingine za kusikitisha toka Mwadui leo jioni. Habari hizi ni kuwa umetokea wizi wa ajabu, maana almasi zote zilizokuwa tayari kusafirishwa kwenda kwenye masoko yake zimeibiwa!"

"Zimeibiwa? Saa ngapi?"

"Anasema ni kati ya saa kumi na saa mbili usiku huu!"

"Kwa hiyo inaonekana majambazi hawa wameamua kuchukua kwa mara ya mwisho na kukimbia."

"Hata mimi nafikiri hivyo hivyo."

"Nafikiri ndiyo sababu Khasimu alinieleza kwamba nifungashe vitu." Amanda alinieleza.

"Nadhani walikuwa wamefanya mpango wa kuziiba hizo almas halafu watoroke nchi za nje."

"Hiyo ni kweli kabisa na vile vile Chifu kanieleza kuwa wale watu uliompigia ripoti watiwe ndani chini ya usalama anashangaa kupata habari kuwa wote hawaonekani na wala haijulikani wako wapi. Mbinu za kila aina zimetumiwa na idara ya upelelezi, Polisi lakini hawaonekani kabisa".

"Ahaa. Sasa naanza kupata mwanga mkubwa. Hii ina maana kuwa wote wameondoka kuja Maganzo kugawana hizi almasi halafu kila mtu aangalie usalama wake, baada ya kuona karibu watashikwa. Hii ikiwa ni kweli lazima wataonana mahali fulani hapa mjini au wameshaonana au wanaonana saa hizi".

"Vile vile kumbukeni kuwa Khasimu alisema kwenye simu anamtegemea Mzee leo saa nne." Amanda alitukumbusha.

"Kwa hiyo hii inazidi kudhihirisha kubuni kwetu. Na kama hata Mzee wao yuko hapa hapa bila ya shaka inabidi tujitoe mhanga na tulikamate hili kundi kabla halijasambaa. Au unasemaje Patrick?"

"Itabidi tuwe tayari kupambana na Elungata. Maana nahisi huyu Elungata ambaye ni Joel tu aliyewahi kusikia sauti yake, huenda ndiye wanamwita Mzee. Kwa hiyo ndiye kichwa".

"Bila shaka, lazima tupambane naye. Lililopo sasa ni kufanya mpango wa namna ya kuwasaka watu hawa",

"Mimi ninavyofikiria, lazima tumkamate Khasimu na Pweke kwanza. Hawa watu wawili ndio watakaotupeleka hata kwenye kichwa".

"Sawa Patrick, Khasimu alikuwa amemchukua Amanda kati ya saa sita sasa ni saa ngapi?"

"Saa saba na nusu." Amanda alijibu.

"Kwa hiyo atakuwa amesharudi nyumbani halafu atakuwa amemkuta Amanda. Hii itamfanya acheleweshe mipango yake kwani hatajua Amanda yuko wapi. Na kwa vile anampenda sana, atajaribu kumtafuta na hii itatupa sisi nafasi ya kuweza kumpata",

"Milimweleza ndugu Mbogo awe hapa kabla ya saa nane unusu, ikiwa hatakuwa amefika ina maana kuwa jambo fulani limemtokea na itabidi kumfuata kwa hiyo mimi naonelea tujilaze kwa muda huu mchache wa saa moja unaweza kutusaidia kupoteza usingizi mpaka hiyo saa nane unusu"

"Sawa Patrick nafikiri nyinyi watu wawili mnahitaji sana huo usingizi hasa Amanda ambaye hakuzoea kukaa macho hadi saa hizi".

"Na wewe pia lazima ukumbuke bado unaumwa kwa hiyo wote hatuna budi kupata usingizi kabla ya mapambano dhidi ya hawa majambazi hayajaanza" Amanda alisema.

Tulizima taa tukajilaza mimi kichwa kilikuwa bado kinanigonga sana lakini ilinibidi kujitahidi niweze kufanya mapambano ya mwisho kwa hawa majambazo, Mambo haya yalinikera sana kuwa sikuweza kupata usingizi mnamo saa nane na dakika ishirini mlango wa chumba uligongwa, bastola mkononi, Patrick alienda kuufungua.

"Uko salama", aliuliza huku akiwasha taa.

"Salama".

Sisi wote tukaamka na kukaa.

"Itabidi tuondoke hapa mara moja wanatutafuta", alisema Wilfred Mbogo.

"Wamejuaje?" Niliuliza.

"Nitawaeleza njiani watafika hapa wakati wowote".

Tulichukua vitu vyetu na mara moja tukawa tunaondoka. Patrick alinipa bastola mbili zenye kiwambo cha kunyamazisha sauti.

"Mimi nafikiri tubane tuwasubiri. Tukiwa na bahati ya kushika mmoja wao anaweza kutupeleka mpaka kwa huyo wanaemuita mzee", nilishauri.

"Sawa, lakini kama ni hivyo itabidi Amanda atusubiri mahali fulani kwani panaweza kutokea mapigano makubwa sana", Patrick alishauri.

"Hata kidogo na mimi lazima niwe katika hayo mapambano mpaka nione mwisho wake. Nikifa kwa ajili ya Joel nitakuwa nimekufa kifo cha fahari, Niko nanyi mpaka mwisho mtake msitake".

"Haya mama ni mapenzi yako", nilimjibu.

Kabla hata Wilfred hajaanza kutueleza gari likatokea kwa kasi lakini lilikuwa bado mbali kidogo. Nafikiri ni hao, Wilfred alipiga kelele.

"Wote kwenye majani", niliamrisha.

Karibu na nyumba kando ya barabara kulikuwa na majani marefu basi tulijificha humo gari lilikuja kasi lilipofika karibu na hiyo nyumba likafunga breki na watu wote watano wakatoka na bastola zikiwa mikononi.

"Ila Willy na Amanda wanahitajiwa kwanza". Mmoja wao aliwaeleza wenzie.

Kila mmoja akachukua sehemu yake tayari kwa mashambulizi, watatu walibaki nje wawili wakaingia ndani. Wote tulikuwa tumelala karibu karibu. "Patrick unaweza kufungua buti ya hiyo gari?" Nilimuuliza kwa sauti ya kunong'ona.

"Naweza bila ya wasiwasi".

"Mimi nataka niingie kwenye buti ndani nikiwa na bahati wanaweza kunifikisha kwenye watu wenyewe ninaowatafuta".

"Wazo zuri," alijibu mwenzangu. "Hata tukisema tuwaue hawa tutakuwa hatujafanya lolote. Naona twende wote ndani ya buti la hilo gari, Amanda na Wilfred watatusubiri kwa Wilfred".

"Najua mkifanya hivyo safari yenu ni mpaka Shinyanga sasa hivi hakuna muda wa kuelezana niliyosikia. Tuonane Shinyanga Relwe nyumba nambari 13. Mimi na Amanda tutasubiri hapo", Wilfred alitoa rai.

"Oke vizuri," nilikubali.

Gari lilikuwa karibu sana na tulipokuwa, "Nendeni mimi nitawalinda ikiwa watawaona," Wilfred alisema.

Tulinyata na kwa sababu mawazo yao yote yalikuwa ni ndani ya nyumba, tuliweza kuingia ndani ya buti ya kuwashitua. Buti la gari kama alivyosema Patrick lilikuwa kubwa sana, mlikuwa na taili moja na supana. Hewa iliyokuwamo ilikuwa kidogo lakini ingeweza kututosha.

"Wameisha ondoka ndani ya chumba hamna mtu wala kitu," tulisikia mmoja wao akisema, "Twendeni zetu tukatoe habari mara moja, huenda ana wazo au habari za mahali walipo."

Waliingia ndani ya gari na safari ikaanza. Walielekea barabara ya Maganzo. Mara kwa mara tulifungua mlango wa buti kuingiza hewa na kuangalia wapi tulipokuwa. Walipofika Maganzo hawakusimama bali waliendelea moja kwa moja kwenye barabara inayoelekea Shinyanga. Kwa vile walikuwa wakienda kasi sana. Patrick na mimi niliweza kunong'onezana juu ya mpango wetu na tulimuomba Mungu atusaidie.

Kama tulivyokuwa tumebuni gari liliingia Shinyanga mjinina kuelekea barabara iendayo nyumba za watu wa hali ya juu. Kisha gari likasimama na kuzima injini. Mlango wa geti ulifungwa na dereva aliamurishwa kulisogeza mpaka mbele kidogo. Punde milango ikafungunguliwa wakatoka nje.

""Twendeni ndani, wanawasubiri kwa hamu sana", kiongozi wao alisema.

Tuliwangoja waende kwanza. Hatmaye tukainua buti ili kuona kama hakukuwa na mtu. Tulipohakikisha kuwa ni salama, nikashika kifuniko cha buti ili Patrick atoke kwanza kisha nami nikafuata. Bahati mbaya nikagusa debe, likapiga kelele. Mtu wao mmoja aliyekuwa kwenye mlango wa mbele ya hiyo nyumba akaja kuangalia. Sisi tukabana kwenye sehemu ya seng'enge ya ua. Alipokaribia Patrick alikuwa

ameshamzunguka. Akamnyemelea, akamkata 'karate' ya shingo na kufa hapo hapo. Hatmaye akanigeukia na kuniamrisha.

"Nenda sasa, lakini jihadhari sana".

"Hakuna taabu", nilimpa imani.

Nilipitia mlango wa mbele, nikaingia ndani. Nilisikia sauti zinatoka kwa mbali kwenye chumba cha ndani. Nilipotaka kuingia mlango ukafunguliwa, nikabana. Akatoka mtu mmoja na bastola mkononi. Kwa vile hamkuwa na taa kwenye ukumbi, hakuniona.Nikamlisha risasi na alipoanguka nikamvuta. Nikamtupa kwenye magunia yaliyokuwa karibu na hapo.

Nilifungua mlango wa nyumba taratibu.Taa zilikuwa zinawaka lakini hakukuwemo mtu. Nilisikia sauti zikitokea kwenye chumba cha pili yake. Nikazima taa za chumba hiki cha kwanza nikaenda mpaka kwenye mlango wa chumba cha pili. Nikasikia sauti ya kiaskali ikifoka.

"Kwa nini mlirudi. Nendeni mkawatafute mpaka muwapate. La asivyo msirudi watu kumi na wawili hamuwezi kushindwa na watu wawili"

"Tutajaribu" Mwingine alijibu.

"Hakuna kujaribu"

Nilihisi hiyo sauti ya Khasimu maana ilikuwa ya kiaskari hasa.

"Khasimu lazima uende nao mumtafute Willy na Umuue pamoja na mwenziwe" sauti hii moja iliamuru.

"Ndiyo Mzee" Khasimu alijibu kwa sauti ya woga.

"Twendeni" walijihimiza.

Mlango wa chumba nilichokuwemo ukafunguliwa

"Nani alizima taa ?" Khasimu aliuliza.

"Sijui, huenda Saidi" alijibu mmoja wao.

"Washa"

Taa haikuwaka. Nilikuwa nimetoa globu yake. Wakati huo nilikuwa nimebana nyumba ya mlango.

"Hamna globu"

"Nini?"

"Hamna globu"

"Angalieni huenda Willy tayarai yupo hapa" Khasimu alitahadharisha.

Kundi lote lilikuwa humo chumbani na wote walikuwa bado hawajaniona. Vilele hawakuwa wanategemea, hivi hawakuwa tayari. Kwa hiyo nikachukua nafasi ya kumjibu.

"Ndiyo tayari niko hapa Elungata."

"Nikaachia risasi toka kwenye bastola zangu mbili na kuwaua wote, maana wote walishikwa na bumbuwazi.

"Njooni,njooni ndani tumeingiliwa. Willy ndani, tumeingiliwa Willy yuko ndani, mkamateni." Sauti ya kutisha ilisikika.

Nilirukia chumba cha pili. mlikuwa hamna mtu tena kulikuwa na mlango unaoeleka chumba kingine. Nilirudi nyuma bastola ikiwa mkononi. Nikaruka nikaupiga teke na kuingia ndani huku nikiviringika sakafuni. Hamna mtu! Niliposimama tu. Pweke alikuwa tayari amesimama mlangoni na bastola mkononi. Kwa vyovyote vile angeniwahi.

"Weka bastola chini" alihamru.

"Mpelee sebule ile. Mikono juu" Nikaweka mikono juu

"huna ujanja tena!"

Nilipofika sebuleni nikashangaa kumuona Patrick naye amekamatwa amefungwa kwenye kiti na huku damu zikimtoka hovyo. nikajua kwamba tumekwisha.

"He, He unashangaa kumuona mwenzio Patrick? Mtanikoma" hiyo sauti ya kutisha ilisema, "Willy Gamba, huu ndiyo mwisho wako. Wengi wamejaribu wameshindwa. Wewe umejaribu sana, na kwa hiyo ninakupongeza."

"Sina haja ya kupongezwa na wewe".

"Wewe ulijaribu kuingilia himaya ya Elungata, aliyoijenga kwa miaka mingi. Je, Ungeweza?"

Nikasikia sauti zinajibu "Asingeweza!" nikajua ya kwamba majambazi wenziwe walikuwa tayari wamewasili na wote walikuwa hapa Khasimu tu ndiye alikuwa amekufa.

"Leo, Gamba, ni siku ya furaha sana kwangu na vijana wangu. Siku ambayo nimeweza kuichukulia Serikali kiasi cha Almasi inayotoka kwa mwaka mzima. Ni utajiri ulioje! na wakati huo huo Gamba unauawa mbele ya macho yangu nilifikiri kwamba baada ya leo nitaacha shughuli hii. Lakini sasa nitaendelea, maana baada ya kusikia umekufa hakuna hatakayethubutu tena."

"Una kichaa, hujui kuwa wananchi wa nchi hii hawatakata tamaa bali wataendelea kupambana nawe na kundi lako kwa ujasiri na ari zaidi, ili mradi kulinda uchumi wa nchi yao. Hawatakata tamaa kupambana na mtu juha kama wewe. Wengi wataendelea kujitoa mhanga mpaka siku watakayoweza kukuweka mbaroni. Wamenyonywa na wakoloni na sasa wamekataa kuonewa tena. Wakoloni wenyewe wanawaogopa wananchi wa nchi hii. Hawataki kuonewa wala kunyonywa tena sembuse wewe kibaraka chao. La hasha wananchi watakumaliza, na siku hiyo watakugawanya vipande."

"Ha, ha, ha! wewe ndiye mwenye kichaa nini kizuri kuliko pesa? utajiri. Ha ha ha, pesa inanunua kila kitu. hawa wananchi unaowasema hii pesa itawanunua na himaya yangu itakaa milele."

"Wananchi wa nchi hii wanajali utu na kulinda uhuru wao, hawajali fedha. Hao wanaojali fedha ndiyo majuha kama wewe na hao tutawapiga vita na kuwamaliza kama tulivyommaliza mkoloni"

Mpaka dakika hii nilikuwa nasikia sauti tu yeye alikuwa haonekani.

"Kabla hamjaniua nawahakikishia kwamba Elungata na wenzio akina Johnstone MWita, Mashaka Athumani, Samweli Gichuki na Tom Omondili, Pweke na bibi yako Tausi, hujuma za wananchi zinawasubiri".

"Piga magoti mbwa wee!" Pweke aliamuru.

"Kwa kheri Willy Gamba pamoja na rafikiyo Patric. Tangulieni ahera. Elungata anawatakieni maisha mema huko. Mnalipia matendo yenu ya kuniingilia!" Pweke alitoa upanga mkali. Mara akatokea mtu mwingine naye na upanga mkali. akasimama nyuma ya Patrick.

"Nikisema moja mbili tatu mnawachoma moyoni kwa pamoja mmesikia?" Elungata alisema kwa sauti ya ghadhabu.

"Ndiyo Mzee" walijibu kwa pamoja.

Haya moja mbili ta...

Kabla hajamaliza hiyo tatu taa zikazimika. Kufumba na kufumbua nikamrukia huyo aliyekuwa tayari kumchoma Patrick, Pweke alikuwa amenikosa, maana baada ya kuruka tu nikasikia Pweke akiguna.

"Aaa nakufa!"

"Washenzi" Sauti ya Elungata ilisikika.

Huyu mtu niliyekuwa nimemrukia kwa woga aliangukia Upanga huku akitoa kelele.

"Mama wee"

Taa ziliwaka, nikamuona Wilfred Mbogo aliyekuwa sasa ameshaingia chumbani akanitupia bastola, yeye akabaki na bunduki.

"Nilinde nimfungue Patrick," nilimwamrisha.

"Hamna tabu" nilichukua upanga wa Pweke nikakatakata kamba alizokuwa amefungwa Patrick.

"Asante sana Wilfred."

Patrick alishukuru huku bado hana maumivu mengi.

"Amanda yupo nje tumuwahi" Wilfred alinong'oneza kila mtu bastola mkononi, tukatoka nje kwa mapambano na kundi la Elungata.

"Nyumba hii ina milango mitano ya kutokea nje sasa sijui Elungata na wenziwe watatokea mlango gani." alieleza Patric huku akituonyesha mahali ilipo.

"Wewe Wilfred tokea mlango wa uani. Patrick mlango wa pembeni na mimi nitatokea mlango wa mbele"

Wilfred alipiga risasi mbili. na hapo hapo tukaona taa zinazimika kwa upande niliotokea niliruka chini na kujivingilisha, risasi zilipigwa lakini zilinikosa. Nilisikia mlio wa bunduki ya Wilfred tena.

SURA YA NANE

Taa zikawaka. Nikawaona watu wawili kabla hawajafyatua risasi zao, mimi nikawawahi. Upande wa Patrick nikasikia bastola inalia. Baada ya muda kidogo gari likatoka mbio.

"Wanakimbia hao" nilisikia sauti ya Amanda.

niliachia risasi lakini gari likawa linaenda tu.

"Elungata na wenziwe wawili wamekimbia" PatricK alieleza.

"Kwa hiyo watatu wamekufa yule msichana yuko wapi?" niliuliza.

"Hata mimi sijui"

"Mtazame ndani"

"Ok"

Nilisikia mlio wa bunduki upande wa Wilfred na nikasikia msichana akilia.

"Niache. Niache haa haa usiniue"

"Usimuue" nilipiga kelele nikijua ni tausi.

Wilfred. Amanda na Tausi walijitokeza na kisha Patrick.

"Elungata na wenziwe wamekimbia na almasi zote" Tausi alipiga kelele.

"Huna haja nazo sasa.Uhalifu wako leo umefika kikomo"

"Mimi ndiye niliyekuwa opareta wa umeme. Unaonaje?" Amanda alijidai.

"Alaa mimi nilikuwa nashangaa sana, hizi taa zilikuwa zinazimishwa na kuwashwa na nani. Binti umefanya kazi nzuri sana na kweli una nidhamu."

"Mara tukasikia mlio wa gari za polisi 999"

"Tumeegesha gari mbele ya pale barabarani" Amanda alisema.

Haya twendeni tusije tukakutwa na Polisi. Muda wa kuonana na polisi bado.

Tuliingia ndani ya gari, Amanda akanipa ufunguo wote watano tukaingia ndani. Safari kituo cha polisi.

"Mmejuaje huku?" nilimuuliza Wilfred.

"Mlipotoka tu walikuwa wamemwacha mmoja wao basi nikamvizia nikamtwanga halafu tukamlazimisha atulete huku nikamtuma Amanda akachukue hilo gari ambalo ni la kaka yangu tukawafuata. Tulijua tu kuwa mtakuwa katika taabu maana yule mtu alitueleza jinsi hapo mahali panavyolindwa. Basi tukaja pamoja na msaada na robo ya ushujaa wa Amanda ambaye aliweza kupenya mpaka kwenye swichi kuu ya mtambo mkubwa wa kuwasha na kuzimisha umeme".

"Mungu si Athuman", Patrick alisema. Tukawa tumeingia kituo cha polisi. Tulimnyanyua Tausi na kumpeleka kaunta.

"Ofisa wa zamu yuko wapi?"

"Yuko ndani", alijibu Koplo mmoja wa kaunta.

Tulipofika ndani nikamkuta Inspekta wa zamu. Nikatoa kitambulisho changu.

"Mweke huyu mama ndani mpaka utakapopata amri nyingine, Nkuu wa mkoa wa Polisi yuko hapa Shinyanga?"

"Ndiyo yupo."

"Mpigie nyumbani kwake".

Ilikuwa sasa yapata saa kumi na moja asubuhi.

"Hallo", aliita Inspekta.

"Kuna ndugu wa Idara ya Upelelezi, Ndugu Willy Gamba anataka kuzungumza nawe".

"Hallo, Willy Gamba hapa".

"Habari gani?" aliamkia huku sauti ikitetemeka.

"Jambo la kwanza funga barabara zote gari lolote lisiweze kuingia wala kutoka Shinyanga sasa hivi, usichelewe hata dakika moja, na uwaeleze Mwanza na Geita washike kila gari linaloingia toka Shinyanga sasa hivi na wangoje amri nyingine".

"Sawa, asante sana".

"Pili kuna nyumba moja huko Ushirika, Polisi wa 999 wameenda huko, tafadhali wakae hapo hapo mpaka amri nyingine itakapotoka. Wewe tuonane saa moja hapa Kituo cha Polisi".

"Sawa ndugu".

Kisha nilichukua simu nikapiga kwa Chifu. Wakati nangojea simu nikashauri Amanda akapumzike.

"Hata mimi naona hivyo", Patrick alisema.

"Kazi uliyoifanya inatosha, Amanda", niliongezea.

Aliniangalia kwa jicho la mahaba sana.

"Nitakuona tena Willy?".

"Bila ya shaka. Si uko likizo? Basi nenda kashike chumba Shinyanga Hoteli, pumzika mimi nitakukuta hapo".

"Sema sisi", Patrick alitania.

Wote tukacheka.

"Haya, nitasubiri kwa hamu kubwa. Mungu awasaidieni mumkamate Elungata".

"Siku za mwizi ni arobani, nafikiri karibu siku zake zitatimia", Wilfred alisema.

"Nafikiri Wilfred ampeleke halafu aturudie sisi hapa", Patrick alishauri.

"Sawa, Wilfred mpeleke".

Wilfred na Amanda wakaondoka. Inspekta akamshika Tausi mkono ili kumpeleka rumande.

"Mimi mtanifanya nini?" Tausi aliuliza.

"Sisi hatutakufanya lolote, ila wananchi ambao umekuwa unawadhulumu watajua la kukufanya. Sisi tutakupeleka mikononi mwao. Lazima ujuwe kuwa uhalifu haulipi", nilimjibu.

Niliinua simu. Inspekta akamvuta Tausi na kumpeleka rumande.

"Halo Willy hapa".

"Unasemaje?" Chifu aliuliza.

Nilimweleza maendeleo yote mpaka dakika hiyo.

"Kazi nzuri sana", alijibu.

"Tunakuomba uchukue ndege na ufikie haraka hapa Shinyanga bila kuchelewa".

"Kwanini?".

"Njoo kuna mambo mengine ambayo sitaweza kukueleza. Nataka uje uyaone mwenyewe kwa macho".

"Sasa ni saa kumi na mbili kasoro robo. Saa tatu nitakuwa hapo. Tuonane Tanganyika Hoteli."

"Asante sana".

Nikaweka simu.

"Anakuja?" Patrick aliuliza.

"Ndiyo, anakuja".

"Kwanini umemwita?" Patrick aliuliza zaidi kwa kushangaa.

"Na yeye aje apambane na Elungata, tumechoka na sisi".

Wote tukacheka lakini nikajua jibu langu halikumridhisha Patrick.

"Sasa tufanye nini?"

"Tumungoje Wilfred. Yeye ana rafiki hapa na tunaweza, sasa tunaweza kwenda kuoga, tukapumzika kidogo, saa moja tuwe hapa kuonana na Mkuu wa Polisi wa Mkoa".

Mara Wilfred akatokea huku jasho likimtoka.

"Mbona jasho linakutoka hivi?" nilimuuliza.

"Hee bwana, kuna makubwa tena, watu watatu wamekutwa wamekufa ndani ya lile gari alilotoroka nalo Elungata!".

"Upande gani?"

"Karibu na kituo cha mabasi. Ina maana watu wamekufa?"

"Si waliotoroka na Elungata walikuwa wawili na yeye wa tatu?" Patrick alihoji.

"Si kitu cha kushangaza. Polisi wametambua moja wapo za maiti kuwa ni maiti ya Mkuu wa Polisi wa Mwadui."

Hii haikunishangaza sana ingawaje Patrick alionekana na mshangao.

"Tena wameuawa kwa kupigwa risasi kifuani", alimalizia.

"Hii ina maana Elungata amekata shauri kuwarusha wenziwe. Sasa kabaki peke yake na mali yote", nilisema.

Niliingia ndani mpaka ofisini kwa Inspekta.

"Tafuta kama kuna gari lolote lililoibiwa mjini hapa yaani kama kuna mtu amepotelewa na gari lake".

"Sawa ndugu".

"Sisi tunatoka tutarudi hapa saa moja."

Tuliondoka kuelekea kwa rafiki yake Wilfred. Tulioga na kupata chai. Ilipofika saa moja tukaanza safari ya kurudi Polisi. Tulipofika huko nikaenda moja kwa moja mpaka ofisini kwa Inspekta.

"Umepata habari yoyote?" Nilimuuliza.

"Ulipoondoka tu nilituma magari ya polisi 999 matatu lakini sikupata taarifa yoyote ya kuibiwa gari".

"Vizuri".

Nilitoka na kuwafuata akina Patrick ambao walikuwa ndani ya gari.

"Inspekta anasema hakuna gari lolote lililoibiwa".

"Ina maana kuwa Elungata bado yuko Shinyanga kama hakuondoka kwa miguu, jambo ambalo haliwezekani", alisema Patrick.

"Sawa kabisa, hata mimi nafikiri Elungata yuko hapa hapa mjini.

Mara likanijia wazo, moyo wangu ukapiga upesi upesi. Nikaona nifanye kama mawazo yangu yanavyonituma.

"Vipi mbona umeduwaa?", Wilfred aliniuliza.

"Nilikuwa nafikiri Wilfred, asante sana kwa shughuli yote uliyofanya".

Nilitoa kibeti changu, nikatoa fedha.

"Chukua hizi shilingi elfu tatu, iwe nauli yako ya kwenda Dar es Salaam".

"Niende Dar es Salaam kufanya nini?" alidakia kwa kushangaa.

"Fika Dar es Salaam. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Umwone Mkuu wa Polisi wa Tanzania, tarehe kumi na tano mwezi huu. Utakuta habari zako zote huko".

"Habari gani?".

"Utazijua wakati huo. Ni lazima ujivune, maana jina lako litakuwa kwenye vitabu vya mashujaa wa Tanzania kwa sababu umepigana kiume, kuyaangusha haya majambazi".

"Lakini mbona bado hatujamkamata Elungata?".

"Hiyo tuachie sisi. Kazi iliyobaki ni ndogo sana, kwa kusema ukweli imekwisha. Soma gazeti la keshokutwa na utashangaa".

"Haya kwaheri. Mungu akipenda tutaonana".

Tuliagana huku machozi yakitulengalenga. Wilfred aliondoka na gari.

"Ulishafanya mipango au vipi?" Patrick aliuliza.

"Nikirudi tu Dar es Salaam sina budi kufanya mpango, kazi aliyofanya lazima impatie maslahi fulani.

"Sawa, hakika huyu kijana kafanya kazi kama mmoja wetu. Kusema kweli anastahili sifa na tuzo. Twende zetu tukatafute hoteli ya kulala".

"Itabidi tukae hoteli mbali mbali".

"Tupite Shinya Hoteli tuone kana kuna nafasi, halafu twende Butiama. Tukipata nafasi Shinyanga wewe utalala hapo", Patrick alisema huku akitabasamu.

"Kwanini?"

"Amanda yuko huko".

Wote tukacheka.

"Si lazima".

Tukacheka tena.

"Hapana iko sababu, kama nafasi ipo Shinyanga Hoteli wewe utakaa hapo. Utajua baadaye kwa nini".

"Sawa, wewe ndiye bosi".

Wakati tunataka kuondoka tu Mkuu wa Polisi wa Mkoa akafika na gari.

"Umechelewa sana, sasa karibu saa mbili kasorobo", nilimwambia.

"Nilikuwa nachunguza mambo yalivyokwenda. Toka saa zile hakuna gari lililotoka Shinyanga. Magari yote yaliyoingia yamekaguliwa vizuri kabisa. Jambo la kusikitisha tu ni kwamba nimepata habari za mauaji ya Mkuu wa Polisi wa Mwadui".

"Hata sisi tumesikitishwa sana".

"Tunajaribu hivi sasa kutambua maiti zingine zilizokuwemo ndani ya gari".

"Fanyeni hivyo".

"Nimepata simu toka Dar es Salaam kuwa Mkuu wa Polisi atafika hapa mnamo saa tatu".

"Vizuri, lakini sasa tunaomba gari moja", nilimwambia.

"Bila ya wasiwasi chukueni".

"Ukipata habari zozote tuwekee, tutakuja kuulizia".

"Mimi sitatoka, niko hapa hapa namsubiri Mkuu wa Polisi".

Tukaondoka mpaka Shinyanga Hoteli.

"Vyumba vipo?" niliuliza.

"Vipo".

"Hebu nipe kitabu cha wageni niandike".

Nilipewa kitabu. Nikaangalia majina yote yaliyokuwemo. Jina la Amanda lilikuwa chini kabisa, chumba nambari tisa. "Patrick njoo uchague chumba".

Akaangalia majina yote.

"Nachagua chumba nambari kumi, lakini usilie wivu, wewe mwenyewe unayataka".

Tukacheka. Baada ya hapo tukaelekea Butiama Hoteli.

"Kuna vyumba vya kulala?|

"Kimebaki kimoja tu chenye vitanda viwili".

"Sawa, nipe kitabu".

Alinipa kitabu, nikaanza kuangalia. Mara moyo wangu ukaruka kidogo. Jasho likanitoka, nikajikaza mshangao wangu usionekane. Kisha nikajaza kitabu kama ilivyohitajika.

"Mna mizigo?" aliuliza mpokezi wageni.

"Tutaleta".

"Haya, vizuri".

Ilikuwa yapata saa mbili na nusu sasa.

"Twende tukapate chakula cha asubuhi Tanganyika Hoteli wakati tunangoja Chifu afike," nilimwambia Patrick.

"Sawa, hata mimi nasikia njaa sana. umesema jambo la maana sana.

Tulienda zetu Tanganyika Hoteli tukaagiza chakula. Chakula kikaja, tukala kimya kimya, maana kila mtu alikuwa na njaa.

"Lo, mnakula kama kwamba mnangombana na chakula", Chifu alitushtua.

Chifu na Mkuu wa Polisi walikuwa wameingia bila ya kuwaona kwa jinsi tulivyokuwa tunakishughulikia chakula kikamilifu.

"Lo, nyuso zenu vipi, mbona kama mmeraruriwa na chui", Chifu alitania kama kawaida yake.

"Kuna binti mmoja ana kucha huyo, afadhali ya Chui," nilitania.

Tuliinuka na kuwavutia viti.

"Shikamoo", tulisalimu kwa pamoja.

"Marahaba", wote wakajibu kwa pamoja.

Nilimwita mhudumu wa hoteli awahudumie.

"Nasikia mliweka ulinzi gari lisiingie wala kutoka, mbona kiwanja cha ndege mlisahau? Hamfikirii kuwa mtu angeweza kutoroka kwa kupitia njia hiyo?". aliuliza Mkuu wa Polisi.

"Sijui", Mkuu wa Polisi wa Mkoa", nilimjibu.

"willy, huwezi kumjibu Inspekta Mkuu hivyo!" Chifu alinikanya.

"Samahani mzee, nafikiri akili yangu imevurugika sana.

"Kuna zaidi mpaka sasa, kuliko kifo cha Mkuu wa Polisi wa Mwadui?" Mkuu wa Polisi aliuliza.

"Hapana zaidi", nilijibu.

"Sasa mmetuitia nini? Elungata mmeshamshika?" Chifu alifoka kwa sauti ya chini chini.

"Kukujibu maswali yako mawili kwa pamoja bado hatujamshika, tumekuita uje kutusaidia.

"Willy, tusitaniane. Unadhani".

"Basi Chifu, sidhani kama kawaitia hilo. Hata mimi hajaniambia. Nafikiri tungoje, atatueleza anavyofikiri yeye", Patrick aliingilia.

Chifu alisonya kwa hasira, lakini hakunishtusha, maana ndivyo alivyo. Hujiwa na hasira mara moja na kupoa hasa afikiriapo kwamba unajaribu kutaniana na huku yeye akiwa na maana kazi. Tulimalizia kula chakula tukiwa kimya. Tulipomaliza kula na kulipa, nikasimama.

"Sasa twende kwanza hotelini tukazungumze vizuri, hapa si mahali pa kuzungumzia kazi ila mahali pa kula".

"Ndiyo sababu ukawa matata?" Chifu alisema akitabasamu.

Tulipofika Mkuu wa Polisi akasema. "Mimi nafikiria twende tukaelezane kwenye Kituo cha Polisi".

"Sisi siyo Polisi, kama unataka kuchukua maelezo kwenye karatasi za polisi ni..."

"Willy, nilikwambia nini? Mbona unakosa nidhamu!" Chifu alionya tena.

"Kweli, samahani nasikitika sana. Nafikiri sijalala vizuri siku nyingi. Kichwa changu bado hakifanyi kazi sawaswa".

"Basi twende zetu huko hotelini kwake anakokusema." Mkuu wa Polisi alisema.

"Mna gari?" niliwauliza.

"Tulikuja na taksi kutoka kiwanja cha ndege, tukairuhusu iondoke baada ya kufika hapa".

Patrick aliwafungulia milango ya gari. Niliendesha mpaka Butiama Hoteli. Tulitelemka tukaingia hotelini. Kufika tu mapokezi akanidakia.

"Mizigo iko wapo, kama huna mizigo hupandi juu!".

Nikatoa kitambulisho changu.

Akanipa funguo huku akitetemeka.

"Orofa ya kwanza kiko mkono wa kulia".

Tulipoanza kupanda ngazi tu nikatoa bastola yangu na Patrick naye bila ya kuchelewa akatoa bastola yake, Chifu na Inspekta Mkuu wakatazamana bila ya kusema lolote na kumeza mate.

SURA YA TISA

Tulipofika orofa ya kwanza nikaangalia vyumba. Chumba nilichokuwa nakitafuta kilikuwa upande wa kushoto. Nilielekea upande huo nao wakanifuata. Nilipofika karibu na chumba nilichokuwa nakitafuta, nikamuonyesha Patrick ishara ya kuwakinga Chifu na Inspekta Mkuu iwapo kutatokea taabu yoyote. Nilipowaangalia Inspekta Mkuu akatoa kitambaa na kuanza kufuta jasho. Nilipokuwa sawasawa na mlango nikarudi nyuma kwenye ukuta bastola mkononi. Nikaruka na kuupiga mlango kwa magoti yote mawili. Mlango ukafunguka nikaangukia ndani.

"Usisogee popote, kaa kama ulivyo," nilimwamrisha na huku nimemlenga bastola, "Patrick walete wazee ndani".

Patrick akiwa na bastola mkononi aliwangiza Chifu na Inspekta Mkuu ndani. Wote walipoingia wakashtuka, wakashikwa na bumbuwazi.

"Oswald Mengi umefika huku lini?" Inspekta Mkuu aliuliza kwa mshangao.

Kabla hajajibu nikasema, "Onaneni na Oswald Mengi Elius Elungata Kamishna Mkuu wa Polisi na mkuu wa Majambazi wa wizi wa almasi".

"Mwongo, mwongo ananisingizia ," alipiga kelele huku akitetemeka kwa woga.

Chifu, Patrick na Inspekta Mkuu walikuwa bado katika mshangao.

"Chifu, nilikuita kusudi uje ujionee mwenyewe jinsi baadhi ya viongozi wetu walivyo waovu. Ni jambo la kusikitisha sana kufahamu kuwa Kamishna Mkuu wa Polisi ambaye anapaswa kuupiga vita ujambazi ndiye Mkuu wa majambazi".

"Mimi sielewi hata kidogo", Patrick alidai.

Chifu na Inspekta Mkuu wote walionyesha mshangao!

"Ni mwongo ni mwongo mkubwa. Anataka kunisingizia tu. Kashindwa kumtafuta Mkuu wa majambazi. Ananisingizia mimi. Nimekuja kwa ajili ya kazi hii hii huku nikiwa nimemwacha mke wangu mahututi. halafu unakuja kunisingizia kiasi hiki. Mimi niwe Mkuu wa majambazi. Wewe Willy una kichaa? Kichaa", Oswald Mengi alisema kwa ukali.

"Kama tungechelewa kidogo, Elungata angepotea kabisa na tungeonana na Oswald Mengi peke yake, akidai kuwa baada ya kupata habari kuwa Inspekta Mkuu na

Chifu wako hapa na yeye akaja. Wote tungeamini na Elungata asingepatikana kamwe kwa sababu Elungata ndiye Oswald Mengi!"

"Kweli kabisa nimekuja kupigana nanyi bega kwa bega dhidi ya majambazi," alipiga tena kelele.

Wote walikuwa wapo na mshangao.

"Chifu kaeni kwenye viti"

Mlikuwa na viti viwili Patrick akaegemea kwenye mlango huku bastola yake ikimlenga Mengi. Mimi nikakaa juu ya meza, bastola yangu ikimlenga vile vile.

"Nitawaeleza mambo yote toka mwanzo mpaka mwisho"

Wote wakaa chini wakiwa bado wameshangaa la kusema hawana!

"Katika mashimo ya almasi ya Mwadui kumekuwa na wizi mdogo mdogo wa almasi, ambao ulianza miaka mingi toka hata wakati wa ukoloni na nyote mnajua. Wizi ambao ulianza kushtusha serikali umetokea miaka miwili tu hivi iliyopita. Na kama mnakumbuka, Mengi alikuwa mkuu wa Polisi wa Mwadui kwa miaka mitano na wakati wote huu wizi ulikuwa ni mdogo mdogo tu.

Miaka miwili na nusu iliyopita, Mengi alipandishwa cheo na kuwa kamishna Mwandamizi wa Polisi na kuhamishiwa Dar es Salaam, Miaka yote hii alipokuwa Mwadui alikuwa anapanga jinsi gani anaweza kuanzisha wizi wa almasi, lakini akaona kuna hatari ya kuweza kugunduliwa. Wakati amepanda cheo na kuhamishwa ndipo akapata nafasi. Na kama mnakumbuka yapata miaka miwili na nusu sasa toka atoke Mwadui na ni baada ya miezi sita tu ndipo wizi kabambe ulipoanza.

"Mkuu wa Polisi wa Mwadui, ambaye sasa hivi ni marehemu alihamishiwa Mwadui miaka miwili iliyopita na kama sitakosea Mengi ndiye aliyependekeza jina lake na akapendekeza kuhamishwa kwa Mkuu wa Polisi aliyekuwa amekaa hapo muda mfupi tu Mengi alimpa huyu marehemu mipango yake na jinsi ya kuitekeleza.

"Na huko Mwadui alikuwa na kijana wake Khasimu Omari ambaye alikuwa Inspekta Mwandamizi na alimwelekeza akafanya naye kazi bega kwa bega chini ya mwongozo wake. Kwa hiyo hii iliwapa nafasi nzuri sana ya kuweza kuendesha wizi bila wasiwasi. Na kwa upande wa Mengi ingekuwa vigumu sana mtu yeyote kumfikiria. Vile vile ingekuwa vigumu kuwashika, maana mara utokeapo

uchunguzi ilibidi yeye Mengi ahusike katika kuutekeleza na hivyo aliweza kujua mbinu za kuangamiza uchunguzi wa hali yoyote kabla haujafika mbali.

Khasimu Omari alikuwa anajuana na Pweke ambaye kwa mara nyingi alikuwa anaendesha wizi mdogo mdogo na kwa jinsi ile yeye ndiye aliyekuwa akijua masoko ya wizi wa almasi za wizi. Kwa hiyo upande wa soko ilikuwa kazi ya Pweke ambaye alijuana na wale watu niliowapa majina muwakamate ma kuwaweka chini ya ulinzi, maana hao ndio waliokuwa wakala wa almasi kwa wafanya magendo kwa nchi za nje. Kwa jinsi ile mambo yalienda vizuri bila ya wasiwasi maana kila upande ulikuwa na mpango thabiti.

"Kwa hivi, Chifu kila alipokuwa akituma wapelelezi, walikuwa hawawezi kufua dafu, maana habari zilijulikana tu baada ya kuondoka hapa. Wote akina Jack Mwile, Makungu Majula na wengineo waliweza kuuawa kwa urahisi kwa sababu hiyo hiyo. Mbile katika uchunguzi wake alifika mbali kiasi cha kujua kuwa mtu aitwae Elungata ndiye aliyekuwa Mkuu wa majambazi, lakini aliuawa kabla hajaweza kuleta ripoti kamili. Kwa bahati aliweza kunifikishia ujumbe juu ya hili jina.

"Kila uhalifu una kikomo chake, maana itajatokea siku moja atafanya kosa kidogo na ndipo atajisaliti.

"Wakati mimi naondoka, watu waliojua juu ya kuondoka kwangu, ni wewe Chifu, Inspekta Mkuu, Waziri wa Mambo ya ndani ya nchi, na bila ya shaka, Mengi ambaye Inspekta Mkuu alienda kumweleza akiwa kama msaidizi wake mkuu.

"Kosa la kwanza alilofanya Mengi ni kuwa mimi nilipofika tu Mwanza, habari zangu zilikuwa tayari zimefika, maana sikukaa hata masaa mawili kabla ya chumba changu hakijakaguliwa na hali nilikuwa nimebadilisha sura na jina. Ingekuwa vigumu mtu yeyote nje ya hao niliowataja kunitambua. Kwa hivi mara moja nikaanza kuhisi kuwa kuna mtu miongoni mwetu aliyekuwa na uhusiano na haya majambazi. Kwa hiyo nikaanza kujihadhari sana huku nikijaribu kumtafuta huyu mtu kati yatu.

"Jambo lilonidhihirishia kabisa kuwa huyu mtu yu miongoni mwetu ni wakati George alipokuja, kwani na yeye kabla hajafika habari zake zilikuwa zimefika. Na wakati huu watu walikuwa wanajua habari za safari ya George ya Mwanza, Ni wewe Chifu na Mengi, maana Waziri pamoja na Inspekta Mkuu walikuwa wamekwenda Lusaka. Kwa hivi ikabidi nichunguze zaidi kati yenu ni nani.

"Mambo yalipozidi kwenda vibaya kwa upande wake Mengi akatoa amri ufanyike wizi wa hali ya juu kabisa na kumweleza Khasimu na Mkuu wa Polisi wa Mwadui kuwa anawasili Maganzo kitu kilichonifanya sasa nimtuhumu Mengi peke yake ni wakati Patrick alipokuja, Habari zake hazikuwa zimefika kwa kuwa Mengi hakujua kuwa Patrick alikuwa akija maana yeye alikuwa wakati huo ameisha omba ruhusa ya kwenda kumuona mkewe aliyepatwa na ajali. Kwa hivi Patrick alipofika hakuna aliyejua.

"Habari kuwa mkewe alikuwa amepatwa na ajali ilikuwa ni uongo. Hii ilikuwa njia ya kutafuta namna ya kuja Maganzo. Kwa hiyo badala ya kwenda Arusha, ambako kweli ndiko mke wake aliko, amekodi ndege ya Tim Air na kuja Shinyanga. Ukitaka kuthibitisha utakuta mtu kwa jina la Ochald Mengi amekodi ndege kuja Shinyanga jana jioni kwani walimtegemea kufika Maganzo mnamo saa nne.

"Alipofika Maganzo na kukuta mambo yameharibika zaidi, akawachukua wenzie mpaka Shinyanga, ambako wangegawana almasi zilizoibiwa jana, halafu kila mtu aende zake. Kwa bahati sisi tukaweza kuwagundua. Kitu kingine kilichofanya nijue kwamba lazima huyu mtu tunamfahamu ni wakati tumeshikwa mimi na Patrick Elungata alikuwa akizungumzia kwenye chumba akiwa amejificha na sauti aliyokuwa anaitoa ungejua kuwa ni ya kuiga. Hii ilizidi kunidhihirishia kuwa huenda hisia zangu ni sahihi.

"Watu waliokuwa wakifahamu kuwa Elungata ndiye Oswald Mengi, walikuwa watu wawili tu, Khasimu Omari na Mkuu wa Polisi wa Mwadui kwa hiyo kuuawa kwa Khasimu Omari kwenye hiyo nyumba huko Ushirika ilimpa Mengi wazo la kutoroka na hao wengine, sisi tubaki tuwamalize wale waliobaki ndani ya ile nyumba. Lakini yeye akawamaliza hao alioondoka nao akiwemo Mkuu wa Polisi wa Mwadui, ambaye ndiye peke yake aliyebaki akimjua yeye ni nani.

"Alijua kwamba kaisha waua hao atakuwa amebaki na almasi zote na angeweza kujitokeza kama vile anavyosema sasa kuwa naye amekuja kuona mambo yanakwendaje. Lakini kwa vile nilikuwa nimeisha muhisi, nilipata habari za kuuawa kwa hawa watu ndani ya gari akiwemo huyo Afisa wa Polisi. Nikajua karibu tunapata mzizi wa tatizo letu ndipo nikaomba ufike ujionee mwenyewe.

"Kwanza nilifikiria kwamba atatoroka. Lakini nilipoambiwa kwamba hakuna gari lililotoka, nikajua dhahiri kuwa bado Elungata yumo Shinyanga. Kusudi niweze kuthihirisha mambo yote niliyokuwa nimekisia, nilienda kila hoteli nitafuta jina linalofanana kidogo na Oswald Mengi. Kwa bahati nilipofika hapa Butiama Hoteli kuangalia katika rejista. Nikakuta jina la Ochard Mengi. Hii ikanidhihirishia kuwa

makisio yangu yalikuwa sawa. Maana jina la Ochard Mengi ni kidogo sawa na Oswald Mengi.

"Chifu, hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa. Sasa kutaka kukudhihirishia asilimia mia moja kuwa yote niliyosema ni kweli bila ya kumsingizia mtu unayemtafuta ni yeye, subiri. Patrick mwangalie, akileta ujanja wowote piga risasi".

Nilifungua kabati la nguo la humo chumbani. Nikakuta hicho nilichokitaka, kisanduki kidogo cheusi.

"Wewe mshinzi sana. Willy, umenimaliza", Mengi alisema.

Nilifungua hicho kisanduku, ambacho ni cha gharama sana, kikiwa na mifuko ya siri mingi ndani. Katika mfuko mmoja wa siri nikakuta nilichokuwa nikitafuta. Nilitoa mkoba uliojaa almassi tele, zilizokwishapigwa muhuri tayari kwa kusafirishwa ng'ambo.

"Kweli kikulacho ki nguoni mwako". Chifu alisema kwa masikitiko makubwa.

"Piga simu hapo chini ita polisi 999," Inspekta Mkuu alimweleza Patrick.

Patrick akaondoka kwenda kuita 999.

"Kikulacho ki nguoni mwako ni kweli Chifu. Mtu kama huyu anayestahili kulinda uchumi wa wananchi, yeye mwenyewe anakata shauri kuwanyonya na kuwatesa. Ningekuwa na madaraka mtu kama huyu ningemweka hadharani wananchi wenyewe watoe hukumu", alimalizia.

"Mimi nafikiri kuna haja ya kufanya marekebisho katika ngazi zote za uongozi. Kila kiongozi amulikwe maana ni afadhali kuwa na watu wa kawaida elfu moja waovu kuliko viongozi au hata kiongozi mmoja mwovu", alisema Inspekta Mkuu.

"Lililopo sasa ni kuishauri serikali ifanye uchunguzi na iwapo kuna kiongozi anayeonekana msimamo wake ni wasiwasi basi aachishwe uongozi. Wale wanaobaki wapigwe msasa, waweze kuelewa wajibu wao kwa wananchi ni nini, wajibu kwa kazi waliyokabidhiwa na wananchi ni nini. Watoe tamaa ya kujinufaisha wenyewe bali wajitoe mhanga kwa faida ya taifa zima. Jambo la huyu Mengi litasikitisha wengi lakini imekuwa fundisho kwa serikali na wananchi kwa ujumla, kuwa kati ya viongozi wenyewe wa nchi hii, yamo majambazi nambari moja. Mara kwa mara watu hufikiria watu wadogo. Lakini tokea sasa tutakaza macho kwa watu wakubwa, maana hawa ndiyo rahisi sana kuangusha taifa hili

kiuchumi. Ni aibu kwa mtu kama huyu", Chifu alisisitiza huku machozi yakimlengalenga.

"Nitahakikisha kuimarishwa kwa Jeshi la Polisi kikamilifu, na naomba iwe hivyo katika sehemu zingine kwa manufaa ya wananchi. Ni jambo la kusikitisha sana, maana nilimwamini sana Mengi, ni sikitiko lililoje!".

Wakati huo huo polisi wakafika pamoja na Patrick.

"Mnaweza kuchukua wiki moja na kupumzika", Chifu alituambia.

"Asante sana", tulishukuru.

MWISHO